
Haliuzwi
DESEMBA 23, 2025
/islamicftz
Rajab 2 1447
# IMAAN
ISSN 5618 - NO. 563
Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Mufti wa Uganda ataka kuimarishwa kwa elimu ya zaka kukabili umaskini



# Waislamu msikose fursa hizi Misk ya Roho


- Ni Jumamosi Desemba 27, 2025, Diamond Jubilee saa 2 hadi 10 alasiri
- Masheikh waanza kuwasili



## Nahdi ajibu wanaodai The Islamic Foundation iko kisiasa


## Mamia Moro wajitokeza kambi ya macho ya The Islamic Foundation





## Janabi: Tujipange, misaada ya afya Afrika inapungua

## Mpango wa amani Gaza ni uongo na kashfa!


Kongamano La 4 La
Afrika Mashariki
Diamond Jubilee
Disemba
27
MUHAMMAD
صلى الله عليه وسلم
"MSINGI
WA AMANI"

MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"

Na Ukhti Fatima Ss

# Waislamu msikose fursa hizi Misk ya Roho

## Misk ya Roho inawatoa watu kutoka hatua moja hadi nyingine ya uelewa, ni kongamano lenye athari kubwa na pana sana kuliko tunavyofikiria," Nahdi alisema

Waislamu wameshajihishwa kujitokeza kwa wingi katika kongamano la Misk ya Roho la mwaka huu kwa kutajiwa fursa kadhaa za kuboresha maisha yao ya akhera na duniani.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa taasisi inayoandaa kongamano hilo, The Islamic Foundation, Aref Nahdi na mhamasishaji sheikh Aweso Rajabu Siri katika kipindi maalumu cha TV Imaan kuelekea kongamano hilo litakalofanyika Desemba 27, 2025 katika ukumbi wa Diamond Jubilee.

Mwenyekiti Nahdi aliwataka Waislamu wasiwe wazito kuziendea kheri, hususan kongamano la Misk ya Roho, ambalo sio tu limekuwa likiwatengeneza Waislamu bali pia limebadilisha mitazamo ya wasiokuwa Waislamu dhidi ya Uislamu kutoka hasi na kuwa chanya.

"Misk ya Roho inawatoa watu kutoka hatua moja hadi nyingine ya uelewa, ni kongamano lenye athari kubwa na pana sana kuliko tunavyofikiria," Nahdi alisema.

Nahdi alisema: "Tunaokwenda pale elfu 5 tu lakini lazima mkumbuke kuna watu zaidi ya milioni mbili wanafuatilia kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, sio hapa Tanzania tu bali hata Comoro, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na kote vinakopatikana visimbuzi vya Azam TV na iliko mitandao ya kijamii dunia nzima.

"Kwa hiyo wewe kutia mkono wako pale ukanunua tiketi ya elfu 15, haisaidii kukupatia chakula tu bali inaungana na elfu 15 nyingine nyingi za wenzako kujenga jambo kubwa na lenye manufaa mengi

"Pale, kwanza, umesababisha umma ukutane; kuna kusikiliza mawaidha, kukubadilisha kitabia, kulea vijana kupitia programu ya kujitolea (volunteering) na kukukutanisha na watu ambao hamkuwa mnajuana. Kuna vitu vingi sana pale vinafanyika.

"Wewe mweyewe umeingia kwa shilingi elfu 15 lakini Wallahi ujue pale umechangia Masheikh 6 kuzungumza na watu elfu 5 ukumbini na zaidi ya milioni 2 kupitia TV, redio na vyombo vya mtandaoni, ambako maudhui yatabaki kwa miaka na miaka. Ule ujira unaupata na unaendelea."

### Sheikh Siri

Naye Sheikh Siri, katika nasaha zake alisema fursa kuu iletwayo na Misk ya Roho ni kutengeneza athari chanya ili mtu akifa aondoke kwa namna nzuri ya kuacha faida endelevu.

"Kufa ni kufa lakini utakufaje? Utakufa umeacha athari gani, nzuri au mbaya. Yaani ukiondoka, watu wakuseme kwa lipi?"

> "Kuna watu walichangia (makongamano yaliyopita) na leo hawapo duniani lakini kwa yale waliyoyafanya bado akaunti za thawabu zao bado zinasoma
>
> **Sheikh Siri**

Akifafanua, Sheikh Siri aliwataka Waislamu kutumia kongamano la Misk ya Roho kuacha athari nzuri, kama ambavyo imekuwa kwa makongamano yaliyofanyika huko nyuma hadi lile la mwisho la 2019 ambayo yaliacha athari kubwa na kufaidisha watu. Alisema hata kipindi liliposimamishwa watu waliendelea kufaidika kupitia maudhui yaliyorekodiwa na ndio maana watu waliendelea kukumbuka na kuomba lirejeshwe.

Akitaja athari chanya mahsusi za Misk ya Roho zilizopita, alisema video za mawaidha zilibaki na zinaendelea kutazamwa huku elimu nayo ikiendelea kusambaa – jambo ambalo linafaidisha kwa chumo la thawabu sio tu wafadhili wakubwa na waandaaji bali pia waliochangia kwa kiasi kidogo cha kiingilio.

"Kuna watu walichangia (makongamano yaliyopita) na leo hawapo duniani lakini kwa yale waliyoyafanya bado akaunti za thawabu zao bado zinasoma," alisema Sheikh Siri, akinukuu Qur'an [36:12]: "Hakika Sisi tunawafufua wafu, na tunayaandika wanayo yatanguliza, na wanayo yaacha nyuma. Na kila kitu tumekihifadhi katika daftari asli lenye kubainisha."

Sheikh Siri amehimiza wale wenye uwezo kununulia watu wanaohitaji tiketi ili waende, akitaja kuwa nayo ni fursa adhimu ya sadaka kupitia elimu.

Alisema: "Leo pale kuna mtu ataingia kwa elfu 15 hajui chochote lakini wewe umemnunulia tiketi. Kuna kitu yule mtu anaondoka nacho kinachosababisha awe na mahusiano mazuri na Allah. Huyu kuna kitu umetengeneza katika moyo wake.

"Kwa hiyo kikubwa pale ni kwenda kutengeneza nyoyo. Waliofika pale kama walikuwa waovu, wataondoka pale wakiwa wema. Kwa hiyo tutumie hii fursa ambayo ni ndogo sana ya masaa machache ambayo itatengeneza maisha yetu ya milele."

MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"

Na Ukhti Fatima Ss

# Nahdi ajibu wanaodai The Islamic Foundation iko kisiasa

Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, amekanusha madai ya wakosoaji wa taasisi yake wanaotuhumu taasisi hiyo inaacha dini na inaelemea sana kwenye mambo ya siasa.

Akihojiwa katika kipindi maalumu cha TV Imaan ikiwa ni maandalizi kuelekea Kongamano la Misk ya Roho litakalofanyika katika ukumbi wa Diamond Jubilee, Disemba 27, Nahdi alisema madai hayo si ya kweli.

"Nataka kukwambieni The Islamic Foundation iko vilevile, inafuata misingi ya dini na inafanya maamuzi kutokana na maslahi ya Waislamu," Aref Nahdi alitangazia wadau wa taasisi hiyo.

Nahdi alisema kitu pekee ambacho taasisi hiyo inafanya, na ambacho pengine kinatafsirika vibaya, ni kushiriki katika ujenzi wa jamii bora kwa kufuata misingi ya Qur'an na Sunna.

"Tunapoona kitu ambacho si sahihi kitatuingizia vijana wetu katika zahma; sisi lazima tuzungumze ukweli, tuweke mambo yetu sawa," alisema Nahdi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kituo cha Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri hapa nchini (CIFCA).

Kwa siku za hivi karibuni, taasisi ya The Islamic Foundation imekuwa mstari wa mbele, ikiungana na Waislamu wote na Watanzania wapenda amani, katika kuhimiza amani na kukataza vitendo vinavyopelekea uchafuzi wa amani ya nchi, kama ilivyotokea siku ya uchaguzi Oktoba 29 na masiku machache baadae.

Umekuwa msimamo wa The Islamic Foundation kuwa haki zidaiwe katika njia za amani kwani amani ikitoweka haki nyingi, ambazo tayari watanzania wanazifurahia sasa hivi zitakuwa hazitekelezeki. Mfano mzuri ni pale amani ilipoyumba kipindi cha uchaguzi ambapo haki zilizozoeleka kama za kuabudu na kutembea popote unapotaka, hazikupatikana.

Katika mahojiano hayo, Nahdi alisema taasisi za Kiislamu zingenyamazia yaliyotokea bila kukemea, zingekuwa zimefanya kosa kubwa sana kwa sababu Waislamu ni sehemu ya jamii ya Kitanzania na hivyo wao pia wangeathirika, pengine hata zaidi ya wengine.

Alionya kuwa mara nyingi Waislamu ni waathirika wakubwa kwa sababu ndio walengwa rahisi wa mashambulizi (soft targets) na kupewa majina mabaya.

Nahdi alisema: "Sisi tukifanya kosa, na pengine hata tusifanye kosa bali tunazushiwa; basi kosa hilo linaonekana ni kubwa sana na adhabu yake ni kubwa kuliko watakayopewa wengine wakifanya makosa ya kiwango hichohicho."

Kutokana na ukweli huo, alisisitiza umuhimu wa Waislamu kuwa makini. "Sisi Waislamu lazima tutumie akili. Lazima tuangalie huko tunapokwenda ni sahihi? Na tujue linapotokea jambo, ni sisi Waislamu ndio tunaopata mnadhara makubwa."

Kipekee Mwenyekiti Nahdi alitaka Waislamu wawaamini viongozi wao kwa sababu wao (viongozi) wanaona ambayo Waislamu wa kawaida hawayaoni.

"Sisi (viongozi) tunaona mbali, tunasikia mengi, tunashauriwa vitu," alisema Nahdi na akaonya kuwa maoni yatolewayo mitandaoni lazima yaangaliwe kwa wasiwasi katika nyakati hizi za akili mnemba (AI) ambapo mtu mmoja anaweza kutengeneza akaunti nyingi feki na kuweka maoni ili ionekane Waislamu wamesema.

"Kwa hiyo sisi The Islamic Foundation, kwa wale wanaotuamini na wale wenye mawazo hasi dhidi yetu, lazima wajue kuwa sisi hatutanyamaza kuona jamii yetu inakwenda kuumia. Tutaiongoza, tutazungumza," alisisitiza Nahdi.



MUHAMMAD صلى الله عليه وسلم "MSINGI WA AMANI"
Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania
Mhariri
+255 789 201383

# Karibuni kwenye Kongamano la Misk ya Roho 2025

Zimebaki siku 5 tu kabla ya kufanyika Kongamano kubwa la Kida'awa la Afrika Mashariki lijulikanalo kama 'Misk ya Roho' siku ya Jumamosi Desemba 27, 2025 katika ukumbi wa Diamond Jubilee, jijini Dar es Salaam.

Hili ni kongamano linalohudhuriwa na maelfu ya watu kutoka jiji la Dar es Salaam na viunga vyake, mikoa mbalimbali ya Tanzania pamoja na nchi za jirani, ukiachilia mbali halaiki ya watu inayofuatilia matangazo yanayorushwa mubashara katika vituo mbalimbali vya runinga na redio duniani kote.

Kuna sababu anuai zinazoonesha umuhimu wa Waislamu na wasiyokuwa Waislamu kuhudhuria kongamano hili ambalo kwa kiasi kikubwa litachangia kuchagiza mwamko wa umma wa Kiislamu na jamii kwa ujumla juu ya umuhimu na jukumu la kutunza amani.

Mbali ya kongamano hili kuzungumzia zaidi amani, pia linaweza kuwa jukwaa (platform) la kuchochea masuala mengine muhimu, kama vile kutengeneza mtandao wa marafiki wazuri ambao mnaweza kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kiuchumi, kijamii, na kadhalika.


Kwa maana hiyo, kongamano hili pia ni uwanja wa kujenga undugu wa kiimani. Kwa maneno mengine, tunaweza kusema Misk ya Roho ni jukwaa huru kwa walinganiaji wa kada tofauti kutoka Afrika Mashariki kubadilishana uzoefu wa kiutendaji linganifu katika tasnia ya da'awa kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki.

Tunapoangazia umuhimu wa kongamano hili ni vyema pia kuyatupia macho manufaa yapatikanayo katika mada zinazowasilishwa ambazo kwa kiasi kikubwa zinaigusa jamii moja kwa moja na zinalenga kujenga mustakabali mwema wa jamii zetu.

Kando na ulinganiaji, kongamano la Misk ya Roho pia ni sehemu mbadala ya Waislamu kustarehe na kufurahi katika namna ambayo Mwenyezi Mungu anaipenda na kuiridhia, tofauti na ilivyozoeleka ambapo sehemu nyingi ambazo vijana wanapenda kufurahi kwazo ni sehemu batili na potofu.

Ni kheri iliyoje kwako wewe Muislamu kuhudhuria katika kikao ambacho ndani yake anatajwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Bila shaka ni jambo zuri lenye manufaa ambalo hakuna miongoni mwetu anayetamani kukosa kheri zake.

Amesema Imam Hasan al–Basri (Allah amrehemu): "Dunia yote ni kiza isipokuwa Majaalis Al–Ulamaa (vikao vya wanachuoni)." Hivyo, tunatoa shime kwa Waislamu na Watanzania wengine kuhudhuria katika kongamano hili ili kufaidika na mada zitakazowasilishwa siku hiyo.



Ukumbi wa Diamond Jubilee.

Misk ya Roho
MWAKA 1447H/2025

Kongamano La 4 La Afrika Mashariki

The Islamic Foundation
المؤسسة الإسلامية

# VITUO VYA TIKETI

**1 ABDULRASHID SAID 0692 600 289**

Wakazi wa Homboza, Chanika yote, Mongo la ndege, Kivule na maeneo ya jirani wafike Masjid Lijumaa Gongo la Mboto

**2 AHMAD UYAI (KINDEGE) 0717 081 199**

Wakazi wa Mikwambe, Kibada Kisarawe Tu, Mji Mwema, na Geza Ulole Vijibweni na maeneo ya jirani wafike Kigamboni Fery

**3 KANZU POINT 0744 577 577**

Wakazi Kariakoo Mnazi Mmoja, Jangwani, Gerezani na maeneo ya jirani fika city mall barabara ya Morogoro na bibi titi.

**4 USTADH MUSTAFA SALIM 0787 620 235**

Wakazi Wa Temeke, Mtoni, Mtongani, Buza, na maeneo ya jirani wafike Tandika Masjid Irshaad Chihota

**5 MKOMELA A MKOMELA 0784 328 512**

Wakazi wa Kisewe, Mbande, Chamazi, Kongowe, na Vikindu wafike Mbagala Rangi Tatu, Sokoni

**6 WAZIRI SONYO 0714 541 957**

Wakazi Wa Manzese, Mburahati, na maeneo ya jirani wafike Masjid Kichangani Magomeni

**7 PEACE TRAVEL 0763 323 232**

Mkabala na msikiti wa Manyema Dar es Salaam

**8 TASTE ME DESERTS AND CAFE 0757 446 444**

Iliopo Coco beach

**9 DISCOUNT CENTRE 0759 130 000**

Mwenge Natai plaza

**10 TASTE ME MART 0765 333 633**

Iliopo Upanga

**11 RAJABU FARIJALA AMIR WA UMASATA 0784 827 337 na 0715 827 337**

Kwa mahitaji ya kuletewa tiketi popote ulipo

27 Disemba | 2:00 Asubuhi - 11:00 Jioni | Diamond Jubilee - Dar Es Salaam

*"Muhammad ﷺ Msingi wa Amani"*

MEDIA PARTNER'S 2025
azam media | azam tv | ZBC2 | DUA tv | AL-HAJJAR TV | tvImaan Tanzania | Radio Imaan FM | IMAAN NEWSPAPER | IMAAN DIGITAL




HABARI
DAR ES SALAAM

MWANDISHI WETU

# Janabi azitahadharisha nchi za Afrika, misaada ikipungua kwa asilimia 70

Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Profesa Mohamed Janabi, amezitaka nchi za Afrika kuongeza kiwango cha fedha katika bajeti zao za afya ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa misaada ya kifedha unaoendelea kushuhudiwa.

Amesema hatua hiyo ni muhimu kufuatia kujitoa kwa baadhi ya mataifa makubwa wafadhili, yakiwemo Marekani, hali iliyosababisha kupungua kwa misaada ya rasilimali fedha kwa takribani asilimia 70.

Profesa Janabi aliyasema hayo jana, wakati WHO kupitia Ofisi yake ya Kanda ya Afrika (WHO-AFRO) ilipokuwa ikisaini Hati ya Makubaliano (MoU) ya kuimarisha ushirikiano wa kikanda wa afya na Jumuiya ya Afya ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini (ECSA-HC), hafla iliyofanyika katika Ofisi za WHO Tanzania.

> **Msaada wa ufadhili kwa WHO umepungua kwa takribani asilimia 70 kufuatia kujiondoa kwa wafadhili wakuu, wakiwemo Marekani. Kinachobaki sasa ni kwa nchi kujipanga upya na kutenga sehemu kubwa zaidi ya bajeti za kitaifa kwa sekta ya afya ili ziweze kukabiliana ipasavyo changamoto hizi zinapojitokeza.**
>
> Professor janabi

Alisema Bara la Afrika linaendelea kuwa na idadi kubwa ya milipuko ya magonjwa ikilinganishwa na mabara mengine, hali inayohitaji rasilimali fedha nyingi katika kukabiliana nayo.

Hata hivyo, kujitoa kwa mfadhili mkubwa kumesababisha pengo kubwa la kifedha katika sekta ya afya.

"Misaada imepungua kwa asilimia 70. Kilichobaki sasa ni nchi kujipanga upya kwa kutenga bajeti kubwa za afya ili ziweze kukabiliana na changamoto hizi pindi zinapojitokeza," alisema Profesa Janabi.

Alieleza kuwa kupungua kwa misaada hiyo kumeathiri pia rasilimali watu, ambapo idadi ya wataalamu imepungua kwa takribani asilimia 25, hali iliyosababisha baadhi ya wataalamu wenye ujuzi mkubwa kuondoka.

Akitoa mfano wa changamoto walizokabiliana nazo, Profesa Janabi alisema wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa Ebola, WHO ililazimika kusafiri kwa takribani siku tano kufika katika eneo la mbali lililoathiriwa, na ndani ya siku 90 waliweza kudhibiti mlipuko huo licha ya changamoto za miundombinu.


"Tulifanikisha kupeleka shehena mbalimbali za dawa na mahitaji maalum, tukaanza kutoa huduma kwa kutumia jenereta, na sasa tumefanikiwa kufunga mifumo ya nishati ya jua," alisema.

Profesa Janabi alisema magonjwa ya kuhara yanaendelea kuwa changamoto kutokana na mabadiliko ya tabianchi, ambapo karibu nchi 15 barani Afrika zimekumbwa na milipuko ya magonjwa mbalimbali, ikiwemo polio Afrika Magharibi na ugonjwa wa Marburg nchini Ethiopia, ambayoyamedhibitiwa.

Aliongeza kuwa mabadiliko ya tabianchi hayaleti changamoto za kiafya pekee, pia huathiri usalama wa chakula katika nchi nyingi za Afrika.

Profesa Janabi alisema magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanaongezeka kwa kasi, ambapo takribani asilimia 32 ya wananchi wa Afrika wana uzito uliokithiri, hali inayoongeza hatari ya magonjwa sugu kama kisukari.

> **Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazojipanga kukabiliana na mabadiliko hayo. Serikali imeainisha mipango ya kupanua uzalishaji wa dawa kupitia ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi, vivutio vya uwekezaji na mageuzi ya kikanuni, ikiwemo kuimarisha Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA).**



Na abdulrahman Omar
0652 408 924

# Mamia Moro wajitokeza kambi ya macho ya The Islamic Foundation

Mkoa wa Morogoro umeshuhudia mwitikio mkubwa wa wananchi kujitokeza kunufaika na kambi ya matibabu ya kibingwa ya macho ya taasisi ya The Islamic Foundation, huduma ambazo zinatarajiwa kukomboa wananchi wengi wanaokabiliwa na changamoto za uoni hafifu.




Huduma hizo zinatolewa kupitia kambi maalum ya matibabu ya macho iliyoandaliwa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na madaktari bingwa waliobobea kwa ufadhili wa shirika la Muntada Aid la Uingereza na kufanyika Msamvu ilipo Al-Jamih for Mother and Child Health Care.

Akizungumza na wanahabari, Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi, amesema huduma hii inasogeza matibabu ya macho karibu na wananchi hususan wale wanaoishi mbali na hospitali kubwa za rufaa, na kwamba watu 500 wanatarajiwa kufanyiwa.

Mwenyekiti Nahdi, alisema kuwa mwitikio wa wananchi umekuwa mkubwa tangu siku ya kwanza ya zoezi hilo, ambapo zaidi ya raia 900 walijiandikisha, akiongeza kuwa idadi hiyo ni ishara ya wazi ya uhitaji mkubwa wa huduma za macho katika jamii, hali inayothibitisha umuhimu wa kuandaa kambi kama hizo mara kwa mara ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Alieleza kuwa dhamira ya taasisi hiyo ni kuhakikisha kila mwananchi anapata haki ya msingi ya huduma za afya ya macho bila kujali hali yake ya kiuchumi, akisisitiza kuwa afya bora ni nguzo muhimu ya maendeleo ya mtu na taifa kwa ujumla.

Nahdi alisisitiza mara kwa mara katika mazungumzo yake na wanahabari kuwa huduma hizo za matibabu ni bure kwa wananchi wote bila kujali dini, kabila, jinsia wala rangi zao.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, katika kipindi chote cha kambi hiyo, wananchi kwa maelfu kadhaa wanatarajiwa kufanyiwa uchunguzi na kati yao, 500 watakaokutwa na matatizo makubwa ya uoni ikiwemo mtoto wa jicho (cataract) watafanyiwa upasuaji.

Ukiacha wale ambao watafanyiwa upasuaji, wengine watapata matibabu ya kawaida ya dawa na wengine watapewa miwani za kuwasaidia kuona.

Nahdi alibainisha kuwa utekelezaji wa kambi hiyo unagharimu zaidi ya shilingi milioni 100, fedha zinazotumika kugharamia vifaa tiba, dawa, upasuaji pamoja na huduma za madaktari bingwa waliobobea.

Alisema licha ya gharama hizo kuwa kubwa, taasisi hiyo, ikishirikiana na wafadhili, wameamua kubeba mzigo huo ili kuwaondolea wananchi adha ya gharama za matibabu ambazo wengi wao wasingeweza kumudu.

## Lengo kufikia nchi nzima

Wakati huohuo, Mwenyekiti Nahdi amesema huu ni mwanzo tu lakini mipango ya baadae ya taasisi yake ni kufikisha huduma za matibabu ya macho na maradhi mengine nchi nzima.

Alisema, ni lengo la taasisi yake kufikia hususan maeneo ya pembezoni yaliyosahaulika, huku akitoa mfano wa mkoa wa Kigoma.

Taasisi ya The Islamic Foundation, kwa zaidi ya miaka 25 ya uhai wake imekuwa ikitekeleza miradi mingi ya kijamii ikiwemo katika sekta ya afya, elimu, maji na kugusa maisha ya watu kwa namna ya kipekee - ikiwa ni sehemu ya mchango wake katika maendeleo ya jamii na katika kusaidia serikali.

Huduma za macho, katika nyakati hizi, zimepewa kipaumbele kutokana na ongezeko la wananchi wanaokabiliwa na uoni hafifu, hali inayowaathiri katika uzalishaji, masomo na shughuli zao za kila siku.

## Ruzuku kwa taasisi za Kiislamu

Sanjari na hilo, Aref Nahdi ameiomba Serikali kuangalia kwa jicho la kipekee taasisi za kidini za Kiislamu zinazotoa huduma za kijamii kwa kuzipa ruzuku, ili kuziwezesha kuendelea kutoa huduma za afya kwa wananchi wengi zaidi.

Alisema kuwa utoaji wa ruzuku kwa taasisi hizo utaimarisha juhudi za Serikali katika sekta ya afya, hasa ikizingatiwa kuwa taasisi za kidini zimekuwa washirika muhimu katika kuwahudumia wananchi wa makundi yenye uhitaji.

## Machozi ya shukran ya wananchi

Kwa upande wao, wananchi waliojitokeza kupata huduma hizo wameishukuru taasisi ya The Islamic Foundation, baadhi yao wakibubujikwa na machozi kwa kupata maoni ya kurejeshewa uoni wao kupitia matibabu hayo, kwa idhini ya Allah.

Wananchi hao wamesema kuwa kwa muda mrefu wamekuwa wakisumbuliwa na matatizo ya macho lakini walishindwa kupata matibabu kutokana na changamoto za kifedha.

Kwa ujumla, kambi ya matibabu ya macho iliyoandaliwa na taasisi ya The Islamic Foundation imeendelea kuonesha umuhimu wa ushirikiano kati ya taasisi binafsi, jamii na Serikali katika kuboresha huduma za afya, huku ikitoa matumaini mapya kwa mamia ya wananchi waliopata na wanaoendelea kupata huduma hizo muhimu.

رَجَب

# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar
0655 763 580



## Kambi ya matibabu ya macho yanufaisha mamia Moro



Wakazi wa mkoa wa Morogoro pamoja na maeneo ya jirani wamejitokeza kwa wingi ili kunufaika na huduma za kibingwa za macho zinazotolewa na madaktari waliobobea, walioletwa na Taasisi ya The Islamic Foundation, katika zoezi lililoanza leo tarehe 22 hadi 25 mwezi huu.

Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation Aref Nahdi akizungumza na wanahabari amesema kuwa lengo la kuleta matibabu hayo ni kusogeza huduma za afya ya macho karibu zaidi na wananchi, hususan wale wasiokuwa na uwezo wa kufika kwenye hospitali kubwa zinazotoa huduma za kibingwa ambapo katika kambi hiyo ya bila malipo wagonjwa elfu nne wanatarajiwa kuonwa huku miatano wakiafanyiwa upasuaji.












# Mufti wa Uganda ataka elimu ya zaka iimarishwe kupambana na umaskini

Mufti wa Uganda, Sheikh Shaban Ramadhan Mubaje, amewataka masheikh na viongozi wa dini ya Kiislamu nchini humo kuongeza juhudi katika kufundisha zaka, akisema kuwa nguzo hiyo muhimu ya Uislamu imepuuzwa kwa kiasi kikubwa, jambo linalochangia kuendelea kwa umaskini katika jamii ya Kiislamu.

Mufti Mubaje alisema Waislamu wengi wenye uwezo wa kutoa zaka hawatekelezi wajibu huo kwa sababu ya ukosefu wa elimu sahihi, hali inayodhoofisha juhudi za kusaidia masikini, yatima na makundi mengine yenye uhitaji mkubwa.

Alitoa kauli hiyo wakati wa hafla iliyoandaliwa na shirika la misaada la Kiislamu la UMMAH, iliyofanyika katika ukumbi wa swala wa Msikiti wa Taifa uliopo makao makuu ya Uganda Muslim Supreme Council mjini Old Kampala.

Mufti alisema zaka si ibada ya hiari bali ni wajibu wa msingi kwa Muislamu mwenye uwezo, na akasisitiza kuwa kutotekelezwa kwake kunapunguza nguvu ya mshikamano wa kijamii ndani ya Umma.

Aliongeza kuwa zaka ikifundishwa na kusimamiwa ipasavyo, inaweza kuwa nyenzo madhubuti ya kupunguza umaskini na kusaidia maendeleo ya jamii.

Alitoa wito kwa viongozi wa misikiti na walimu wa dini kutumia mimbari na madarasa kuelimisha waumini kuhusu hukumu, malengo na faida za zaka, akisisitiza kuwa jukumu hilo ni la msingi katika uongozi wa Kiislamu.



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323



# Uhaba wa maji ni uzembe wa wanadamu au maamuzi ya Mola?

Katika siku za hivi karibuni, jamii nyingi zimejikuta zikikabiliwa na tatizo kubwa la uhaba wa maji. Mvua zimechelewa kunyesha, vyanzo vya maji vimekauka, mito imesinyaa, na visima vingi havitoi maji kama ilivyokuwa awali. Hali hii imeibua maswali mazito: Je, tatizo hili limesababishwa na uzembe wa idara za maji na mainjinia wanaoketi ofisini, au ni mtihani na onyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu?

Kwa mtazamo wa Kiislamu, jambo la kwanza ni kukiri kwamba mvua ni riziki kutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee, si matokeo ya teknolojia wala mipango ya binadamu peke yake. Qur'ani Tukufu inatukumbusha wazi katika Sura al-Mulk, Aya ya 30: "Sema: Je, mmeona ikiwa maji yenu yatatoweka ardhini, nani atakayekuleteeni maji yanayobubujika?"

Aya hii inaweka wazi ukweli usiopingika: mamlaka ya mwisho ya maji iko mikononi mwa Allah. Mwanadamu anaweza kuchimba visima, kujenga mabwawa na kusimamia mifumo ya maji, lakini hawezi kulazimisha maji yatoke ardhini bila idhini ya Muumba.

Hata hivyo, Uislamu hauondoi kabisa wajibu wa mwanadamu. Kinyume chake, unatukumbusha kwamba uzembe, dhulma na uharibifu wa mazingira ni sababu zinazochangia adhabu na kunyimwa baraka, ikiwemo mvua.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) amesema katika hadithi: "Hakika watu hawanyimwi mvua isipokuwa kwa sababu ya dhambi zao." (Imepokewa kwa maana katika vitabu vya hadithi)

Katika hadithi nyingine, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alieleza kuwa miongoni mwa sababu za kukosa mvua ni kuenea kwa dhulma, kutotoa zaka, kutoweka kwa amana na uzembe wa kutekeleza haki za Allah na haki za waja.

Kwa msingi huu, tatizo la uhaba wa maji si la idara za maji pekee, bali ni tatizo la kijamii na kiimani. Jamii inapopotoka, neema hupunguzwa.

Lakini pia, Uislamu ni dini ya uwajibikaji. Hauwakingii kifua watumishi wazembe kwa kisingizio cha "ni mapenzi ya Mungu". Endapo vyanzo vya maji havitunzwi, visima havifufuliwi kwa wakati, miundombinu ikiachwa imechakaa huku mainjinia wakiketi ofisini bila kushuka vijijini na mitaani na kujishughulisha zaidi na kufuatilia Ankara za maji pasipo kuwepo kwa maji, huo ni uzembe unaobeba dhambi na athari zake.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Kila mmoja wenu ni mchungaji, na kila mmoja ataulizwa kuhusu anachokichunga."

Hivyo, wahandisi, watumishi wa idara za maji na viongozi wana dhamana kubwa mbele ya Allah na mbele ya wananchi. Kukosa mipango ya muda mrefu ya kuvuna maji ya mvua, kufufua visima vya kale, na kulinda vyanzo vya maji ni uzembe wa wazi.

Kwa upande wa wananchi, Uislamu unatufundisha kufanya mambo matatu wakati wa uhaba wa mvua; mosi toba ya kweli – kurejea kwa Allah kwa unyenyekevu, dua na Swala ya kuomba mvua (Istisqaa) na kuchukua sababu halali – kuhifadhi maji, kutoharibu mazingira, na kushirikiana na mamlaka.

Mvua inapokosekana, si wakati wa lawama pekee bali ni wakati wa tafakari. Je, tumetimiza haki za Mwenyezi Mungu? Je, viongozi wametimiza wajibu wao? Je, wananchi wametunza neema ya maji?

Kwa kumalizia, Uislamu unatufundisha mizani: Mvua iko mikononi mwa Allah, lakini uzembe uko mikononi mwa wanadamu. Neema ya maji ikikosekana, turejee kwa Allah kwa toba, dua, na sala na wakati huohuo turekebishe mifumo yetu, tufufue visima mapema, tulinde mazingira na tuwawajibishe wanaohusika.

Hakika, maji ni uhai, na uhai ni amana.

Na Said Rajab
0783 650 803

# Mpango wa amani Gaza ni uongo na kashfa!

**Kusema ukweli, mpango wa kusitisha mapigano Gaza ulioanza kutekelezwa Oktoba 10, 2025 siyo amani, bali ni mauaji ya halaiki ya polepole yaliyopewa jina la kupendeza na vyombo vya habari vya Magharibi. Mtazamo wa dunia umepotea.**



# Mpango wa amani Gaza ni uongo na kashfa!



Kusema ukweli, mpango wa kusitisha mapigano Gaza ulioanza kutekelezwa Oktoba 10, 2025 siyo amani, bali ni mauaji ya halaiki ya polepole yaliyopewa jina la kupendeza na vyombo vya habari vya Magharibi. Mtazamo wa dunia umepotea.

Gaza ilikuwa ikivuma hadi ikaacha kuvuma, na sasa Gaza inabanwa pumzi kimya kimya. Mpango wa Trump unaoitwa 'wa amani' wenye vipengele 20, ulioweka msingi wa kusitisha mapigano uliahidi kuwa operesheni zote za kijeshi zitasitishwa.

Rais huyu wa Marekani, Donald Trump, alifikia hatua ya kujisifu kwamba vita imeisha, akisema: "Kwa pamoja tumefanikisha kile ambacho kila mtu alisema hakiwezekani. Hatimaye tuna amani Mashariki ya Kati."

Nchi za Kiarabu zilipongeza, Pakistan iliukaribisha mpango huo, Uturuki iliusifu, na viongozi wa mataifa mengine ya Waislamu walitabasamu mbele ya kamera, wakipeana mikono na Trump, ambaye alidai kwa kejeli ameweza kusuluhisha miaka 3,000 ya mzozo.'

## Usuli

Katika kipindi cha miaka 77 ya uhai wake, taifa la Kizayuni la Israel limekuwa likiitafuna Palestina huku 'mpango' wa sasa wa Trump ukiiacha Israel na udhibiti mkubwa zaidi wa Gaza kuliko ilivyokuwa awali. Huo unaoitwa usitishaji mapigano wa sasa ulianza Oktoba 10, 2025 baada ya zaidi ya miaka miwili ya mauaji ya halaiki, ambayo yamechukua maisha ya takribani watu 70,400 na bado yanaweza kuchukua maisha ya Wapalestina wengine 186,000.

Donald Trump na wasaidizi wake wametangaza 'mpango wa amani' kwamba unatatua maelfu ya miaka ya mgogoro, huku kwa ustadi mkubwa wakipuuza madai ya uongo ya Israel ya hivi karibuni, kwamba Mayahudi na Waislamu wamekuwa katika vita kwa karne nyingi.

Uhalisia ni kwamba, Mayahudi kindakindaki (Orthodox Jews) walio ndani na nje ya Israel wanaipinga vikali Israel na matendo yake huko Palestina, lakini hilo hutalisikia kwenye vyombo vya habari vya Magharibi.

Lakini uhalisia mwingine wa msingi ni kwamba, misaada bado imezuiwa na utawala wa Mazayuni, majeshi ya uvamizi bado yapo Gaza na Palestina, na raia wasio na hatia bado wanaangushiwa mabomu. Trump anatamani uamini kwamba mambo ni shwari kabisa na Gaza kuna amani, lakini huu ndiyo ukweli wenyewe na uhalisia.

## Mauaji ya halaiki yanaendelea

Ukweli ni kwamba, tangu hicho kinachoitwa 'usitishwaji wa mapigano' kilipoanza mapema mwezi Oktoba, Israel haijasitisha kuwaua watu Gaza hata kwa dakika moja. Hakujakuwa na kusimamisha mapigano, hakuna kujizuia kushambulia, na watu wa Gaza hawajapewa hata muda wa kuvuta pumzi.

Zaidi ya majengo 1,500 (idadi halisi inaweza kuwa kubwa zaidi) yamebomolewa katika maeneo ambayo kimsingi hayahitaji tena kushambuliwa. Zaidi ya raia 360 wamauawa, 922 wamejeruhiwa, na miili 617 imefukuliwa kutoka kwenye vifusi, bila shaka wengi wao wakiwa watoto, wanawake na wazee.

Zaidi ya hapo, Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF) limeripoti kwamba watoto wawili waliuawa kila siku wakati wa mchakato wa usitishaji mapigano, na wengine 67 wameuawa baada ya mkataba huo kuanza.

Na hadi sasa Israel bado inazuia misaada ya kibinadamu kama vile chakula, maji na dawa kuingia Gaza. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2025 ni asilimia 10 tu ya dawa na vifaa tiba vinavyohitajika ndiyo iliyoingia Gaza. Malori 90 tu kwa siku ndiyo yaliyoingia ingawa makubaliano yalikuwa malori 600 kila siku. Kwa ulinganifu, mambo yameboreka kwa kiasi fulani, lakini kwa hesabu zote, kiwango cha misaada inayopokelewa Gaza ni kidogo mno ukilinganisha na kile kinachohitajika. Hii siyo amani bali ni baa la njaa linalosimamiwa. Ni kifo cha taratibu.

Hivi sasa Israel inaendelea na mashambulizi ya angani, milio ya risasi za wadunguaji, ukamataji, uvamizi na vizuizi. Mwanahabari wa Gaza, Sara Awad anasema: "Tulinusurika kwenye vita, tunaweza tusinusurike kwenye usitishaji mapigano...Hakuna siku inayopita bila majeruhi, Israel inaendelea kuua kila siku." Ni sahihi kusema kwamba usitishaji wa mapigano Gaza unabaki kuwa uongo.

Sasa tujiulize, hii ndiyo tafsiri ya amani ya nchi za Magharibi, na hiki ndicho watawala wengi wa nchi za Kiarabu wanapanga foleni kusaini? Kwa sababu, chini ya mfumo wa sasa wa ukoloni, ambapo kituo cha mwisho cha kikoloni (Israel) kinalindwa kwa gharama yoyote, hakutakuwa na amani kamwe.

Kama tunavyoona wazi, mauaji ya kimbari Gaza hayakusitishwa, hivyo umma wa Kiislamu duniani haupaswi kutulia kuhusu Gaza!

# رَجَب فتاوى



**SHEIKH**
**Shaaban Mussa**
**0786 272 323**

## Swali: Je, Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa mwanasiasa?

**Jibu:** Iwapo aliyelouliza swali anakusudia neno siasa kwa maana ya kuwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa na sifa za uongozi, uwezo wa kuwaongoza watu, na kusimamia mambo yao kwa namna inayowaletea maslahi yao, basi hilo ni kweli. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa mwanasiasa.

Hata hivyo, neno siasa katika Uislamu halimaanishi ujanja, hila au udanganyifu, bali linamaanisha kusimamia mambo ya watu kwa haki na kwa kuzingatia maslahi yao (siyāsah shar'iyyah). Kwa maana hii, Mtume wa Allah (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa kiongozi na mwanasiasa wa kiwango cha juu kabisa.

Sababu zinazothibitisha hilo ni kwamba aliunganisha dini na uongozi wa jamii, aliongoza kwa haki, hekima na huruma, aliweza kusimamia masuala ya amani, vita, mikataba na mahusiano ya kijamii, na aliongoza kwa lengo la kheri ya dunia na Akhera.

Kwa hiyo, siasa yake ilikuwa sehemu ya Utume wake, si siasa zisizo na haki wala zisizo na maadili.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimkusanyia sifa hizi kwa ukamilifu uliowazidi wanasiasa na viongozi wote waliomtangulia na waliomfuata, hadi siku ambayo Mwenyezi Mungu atairithi ardhi na vilivyomo juu yake.

Yeyote anayechunguza maisha ya Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kabla ya Utume na baada yake, katika nyakati za amani na vita, na katika mahusiano yake na marafiki pamoja na maadui, ataona mambo ya ajabu mno. Haya yote ni kwa sababu Mwenyezi Mungu alimchagua kwa Utume na akamteua kwa Risala, ili awaongoze watu wote na kuiongoza jamii ya binadamu kuelekea kheri ya dunia na Akhera.

Kwa hakika, Manabii waliomtangulia walikuwa wakiongoza kila mmoja kaumu yake pekee, kama ilivyokuja katika Hadith sahihi katika Bukhari na Muslim, na lafudhi ni ya Muslim, kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie) aliyesema:

"Wana wa Israil walikuwa wakiongozwa na Manabii; kila alipofariki Nabii alifuatwa na Nabii mwingine, na hakika hakuna Nabii baada yangu."

Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) upekee wa kutumwa kwa watu wote, akamjaalia uongozi wa wanadamu wote, na akamfanya kuwa mfano wa kuigwa na kila mmoja. Kupitia kwake, aliwatoa watu kutoka gizani kwenda kwenye nuru, na akawakusanya baada ya kutawanyika.

Hata maadui na wapinzani wake walimshuhudia kuwa alikuwa na siasa njema na mipango mizuri. Na kweli ni ile inayoshuhudiwa hata na maadui. Hakika, kila anayemuiga na kujifunza kutoka katika siasa na uongozi wake huwa karibu zaidi na mafanikio.

Kwa hiyo, yeyote anayejishughulisha na siasa za kuwaongoza watu anapaswa kumuiga Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani), ajifunze wasifu wake (Sira), na ajifunze kutokana na siasa na uongozi wake. Hakika Mtume (Allah amshushie rehema na amani) ni mwalimu bora kabisa kwa kila anayelitaka jambo jema.

Kuthibitisha hilo, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Kwa hakika kabisa mna mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anayemtarajia Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho."

(Qur'an, 33:21)

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## Swali: Siku za hivi karibuni kulikuwa na vurugu katika mji wetu zilizoambatana na uharibifu wa taasisi na mali za makampuni mbalimbali. Watu walichoma moto na walichukua mali zilizokuwamo. Nami pia, kwa kufuata mkumbo, nilishiriki na nikachukua baadhi ya vitu. Baada ya kushikamana na dini nimetambua kuwa jambo hilo haliruhusiwi. Nifanye nini kuhusu vitu hivyo?

**Jibu:** Ni wajibu wako kama Muislamu kurudisha vitu hivyo kwa wahusika wake, kwani ulivichukua bila haki. Haijuzu kuvimiliki wala kunufaika navyo.

Iwapo unawajua wamiliki wake, ni lazima uvirejeshe kwao. Na ikiwa huwajui wamiliki wake au huwezi kuwafikia, basi unapaswa kuviwasilisha kwa mamlaka husika kama serikali za mitaa au vyombo vya usalama, au kuviacha katika eneo salama kwa namna inayowezesha wahusika kuvipata.

Pia, ni wajibu wako kutubia toba ya kweli, kuacha kabisa kurudia kitendo hicho, na kumrejea Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa unyenyekevu. Jishughulishe na utiifu Wake, ongeza ibada za sunna, na zidisha istighfari. Huenda Mwenyezi Mungu akakusamehe, akaipokea toba yako, na akakuhitimishia kwa matendo mema.

Aidha, tunakushauri wewe na Waislamu wote—wanaume na wanawake—kujisitiri na fujo zinazokiuka mali, roho na heshima za watu, kwani hazina uhusiano wowote na maadili ya Uislamu.

Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## Swali: Je, kauli hii ni sahihi? Kwamba sisi kama Waislamu hairuhusiwi kabisa kutumia istilahi ya uhuru, hata kama kinachokusudiwa ni uhuru unaojengwa juu ya itikadi ya Kiislamu?

**Jibu:** Kwa hakika, neno uhuru linaweza kutumika likikusudiwa uhuru wa kibinadamu unaohifadhi heshima ya mtu, unalinda utu wake, na kuhifadhi haki na mali zake.

Uislamu umeupa uhuru wa aina hii umuhimu mkubwa, umeweka misingi na kanuni zake, na ulikuwa mtangulizi katika hilo kwa maneno na kwa

رَجَب

## HABARI KIMATAIFA

MAHMOUD NYAMGUMA



# Marufuku ya hijab kwa wanafunzi yaongezeka barani Ulaya

Muungano wa misikiti ya Ghent (VGM) umewasilisha rufaa katika Baraza la Taifa la Ubelgiji kupinga kurejeshwa marufuku ya hijab katika shule za umma katika mkoa wa East Flanders.

VGM wanasema hatua hiyo imekiuka taratibu za ushirikishwaji na inakiuka haki za msingi za wanawake Waislamu.

VGM, kama chombo mwamvuli kinawakilisha misikiti 23 jijini Ghent.

Ubelgiji ina Waislamu wanakadiriwa kuwa kati ya asilimia 6 hadi 7 ya wakazi wote, na katika miji mikubwa kama Ghent, Waislamu wengi wameandikishwa katika shule za umma. Hivyo, athari za sera hii kuwa pana na za moja kwa moja kwa jamii.

VGM imeeleza kuwa marufuku hiyo inafanya wanawake Waislamu kushindwa kuishi na kuonyesha utambulisho wao kwa uhuru, kauli inayoungwa mkono na za haki za binadamu barani Ulaya.

Tafityi zinazoonyesha kuwa sera za mavazi shuleni huathiri zaidi wasichana Waislamu, na katika baadhi ya nchi husababisha ongezeko la kundi hilo kuhamia shule binafsi.

Shirika hilo pia limekosoa vikali kauli za Naibu Mkuu wa Mkoa wa East Flanders, Kurt Moens, aliyedai kuwa alifanya mashauriano na "jumuiya pana ya Waislamu." VGM imesisitiza kuwa haikushirikishwa katika mashauriano hayo. Aidha, VGM imekataa vikali madai kwamba wapinzani wa marufuku ya hijab wanaelemea misimamo mikali.

Wanaharakati wanasema rufaa iliyokatwa inaweza kuweka mwelekeo muhimu kwa sera za elimu Ubelgiji na kanda nzima

# Hali mbaya wafungwa watetezi wa Palestina wanaogoma kula Uingereza

**Familia, wanasheria na madaktari wanaowawakilisha wanaharakati wanaounga mkono Palestina wanaoshikiliwa gerezani nchini Uingereza wameiomba serikali kuchukua hatua za haraka kabla wafungwa hao "hawajapoteza maisha."**

**Ombi hilo lilitolewa katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika London.**

**Wafungwa hao, wanaojulikana kama Prisoners for Palestine, wanaendelea na mgomo wa kula usio na kikomo ulioanza Novemba 2, wakipinga kuzuiliwa kwa muda mrefu bila kufikishwa mahakamani.**

**Baadhi yao wamekuwa kizuizini kwa zaidi ya mwaka mmoja wakisubiri tarehe ya kusikilizwa kwa kesi, wakidaiwa kuhusika katika shambulio dhidi ya kiwanda cha silaha cha Israel kama ishara ya mshikamano na Palestina.**

**Madaktari waliokuwepo wameonya kuwa hali ya wafungwa hao imefikia hatua hatarishi. Dkt. James Smith, daktari wa dharura na mhadhiri, amesema baadhi ya wafungwa wamefika siku 47 bila kula, hatua ambayo kiafya huanza kuhatarisha viungo muhimu vya mwili kama moyo na figo. "Kwa mwelekeo huu, ukweli ni kwamba wanakufa taratibu," alisema. Familia za wafungwa pia zimeeleza hofu kubwa. Shahmina Alam, dada wa mfungwa Muislamu Kamran Ahmed, alisema familia yao inaishi kwa hofu kila siku. Alisema Ahmed anapoteza uzito kwa kasi na hali yake inaweza kubadilika kuwa mbaya wakati wowote.**

**Wabunge akiwemo John McDonnell na Jeremy Corbyn wameahidi kuendelea kushinikiza serikali, wakimtaka Waziri wa Sheria David Lammy kufungua mazungumzo na kutafuta suluhu ya haraka.**




# HABARI KIMATAIFA

MAHMOUD NYAMGUMA

# Marekani kumfukuza aliyerekodi mateso kambi za Uyghur China?




Mwanaume raia wa China aliyesambaza video zinazoonyesha ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya Waislamu wa Uyghur sasa anakabiliwa na hatari ya kufukuzwa Marekani kufuatia kukamatwa na maafisa wa uhamiaji.

Guan Heng (38) aliyekamatwa Agosti yuko kizuizini akisubiri uamuzi wa kesi yake ambapo mama yake Luo Yun ameonesha hofu kubwa kuwa anaweza kurejeshwa China ambako maisha yake yako hatarini.

"Nina wasiwasi mkubwa sana. Akirudishwa China, hali inaweza kuwa mbaya mno kwake," alisema Luo Yun katika mahojiano.

Wakili wa Guan, Chen Chuangchuang, amesema jaji anazingatia uwezekano wa kumpeleka Guan Uganda, nchi iliyokubali kupokea baadhi ya wahamiaji wanaofukuzwa Marekani. Hata hivyo, wakili huyo amesema atapinga vikali hatua hiyo, akisema kuna hatari kubwa ya Guan hatimaye kurejeshwa China.

Mnamo mwaka 2021, Guan alichapisha video ya takribani dakika 20 katika mkoa wa Xinjiang, kaskazini-magharibi mwa China ikionesha maeneo yaliyotajwa kuwa ni kambi za kuwazuilia Uyghur na Waislamu wengine.

Jumuiya ya kimataifa, ikiwemo Umoja wa Mataifa, imeituhumu China kuwazuilia zaidi ya Waislamu milioni moja tangu 2017, madai ambayo Beijing imekuwa ikiyakana.

Taarifa kutoka Tom Lantos Human Rights Commission imeonya kuwa Guan anaweza kuteswa iwapo atarejeshwa China, na kuitaka Marekani kumpa hifadhi.

Mama yake anasema familia yao nchini China pia imekuwa ikihojiwa na mamlaka tangu video hizo zilipochapishwa.

## Waislamu Australia wahofu kuumizwa na 'hasira' za Waziri Mkuu



**Jamii ya Waislamu nchini Australia imeeleza hofu na wasiwasi mkubwa kufuatia tangazo la Waziri Mkuu Anthony Albanese la kuimarisha sheria za kupambana na hotuba za chuki, baada ya tukio la mauaji ya watu 15 katika ufukwe wa Bondi Beach, Sydney.**

**Akinukuliwa na Shirika la Utangazaji la Australia, Albanese alisema Kamati ya Taifa ya Usalama imependekeza kuanzishwa kwa makosa mapya ya jinai dhidi ya viongozi au wahubiri watakaohamasisha vurugu kupitia hotuba za chuki, pamoja na kuongeza adhabu kwa vitendo vya chuki vinavyohamasisha vurugu, hasa kupitia mitandao ya kijamii.**

**Hatua nyingine ni kuifanya chuki kuwa sababu inayoongeza uzito wa adhabu wakati wa kutoa hukumu, kuanzisha utaratibu wa kuyaorodhesha mashirika yanayohusishwa na hotuba za chuki au ubaguzi wa rangi, pamoja na kumpa waziri wa mambo ya ndani mamlaka mapya ya kufuta au kukataa visa.**

**Pia, kikosi kazi cha miezi 12 kitapewa mamlaka ya kuangalia zaidi mfumo wa elimu.**

**Albanese alisema serikali inalazimika kuchukua hatua. "Hakuna serikali iliyo kamilifu, nami si mkamilifu. Lakini tunapaswa kusonga mbele," alisema.**

**Hata hivyo, Waislamu nchini humo wameiambia 5Pillars kuwa hatua hizo zimeongeza hofu ya kushamiri kwa Uislamuofobia na uwezekano wa jamii yao kulengwa kimakosa. Wanawake wanaovaa hijabu wamesemekana kuwa miongoni mwa walio katika hatari zaidi ya mashambulizi au manyanyaso.**

**Chanzo: 5Pillars**

HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU




# Mali za benki za Kiislamu Oman zapanda kwa asilimia 19.5

Muscat – Mali za benki za Kiislamu na madirisha ya benki za Kiislamu katika Usultani wa Oman zimeongezeka kwa kiwango kikubwa, zikifikia takribani riali bilioni 9.2 za Kiomani hadi kufikia mwishoni mwa Oktoba 2025.

Ongezeko hilo linawakilisha asilimia 19.5 ya mali zote za sekta ya benki nchini Oman, na ni sawa na ukuaji wa asilimia 10.8 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka uliopita.

Takwimu hizo zinaonesha kuendelea kuimarika kwa benki za Kiislamu nchini humo, hali inayodhihirisha kuongezeka kwa uaminifu wa wateja na mahitaji ya huduma za kifedha zinazozingatia misingi ya Sharia. Ukuaji huo pia unaakisi juhudi za Oman kuimarisha sekta yake ya fedha kwa kuhimiza mifumo mbadala ya benki inayozingatia maadili na ushirikishwaji wa kifedha.

Kwa upande wa mikopo na ufadhili, kiwango cha fedha kilichotolewa na benki za Kiislamu na madirisha yake kimeongezeka kwa asilimia 10.4, na kufikia takribani riali bilioni 7.4 za Kiomani. Ongezeko hilo linaashiria kuimarika kwa shughuli za biashara na uwekezaji, pamoja na mchango wa benki za Kiislamu katika kusaidia sekta mbalimbali za uchumi.

Aidha, amana katika benki za Kiislamu na madirisha yake pia zimepanda kwa asilimia 11.9, na kufikia karibu riali bilioni 7.3 za Kiomani hadi mwisho wa Oktoba 2025. Ukuaji huu unaonesha kuongezeka kwa imani ya wananchi na taasisi katika mifumo ya benki za Kiislamu, sambamba na utulivu wa sekta ya fedha nchini.

Wachambuzi wa masuala ya kifedha wanasema mwenendo huu chanya unaashiria nafasi inayozidi kukua ya benki za Kiislamu katika mfumo wa kifedha wa Oman, huku zikichangia maendeleo ya uchumi kwa njia inayozingatia maadili, uwazi na usawa wa kifedha.

***Chanzo: Saba***

## Kwa nini sekta benki za Kiislamu Indonesia yakua taratibu, licha ya Waislamu wengi?

**Licha ya Indonesia kuwa na idadi kubwa zaidi ya Waislamu duniani, ukuaji wa benki za Kiislamu nchini humo umeendelea kuwa wa taratibu ikilinganishwa na ukubwa wa soko lililopo.**

**Wachambuzi wa masuala ya kifedha wanasema hali hiyo inatokana na mchanganyiko wa changamoto za kimuundo, uelewa mdogo wa kifedha na ushindani mkali kutoka kwa benki za kawaida.**

**Hata hivyo, kwa mujibu wa Profesa Mohammad Nur Rianto Al Arif, sekta ya benki za Kiislamu Indonesia imefanikiwa kujenga uaminifu na uthabiti, lakini bado inakabiliwa na vikwazo vya ukubwa wa mitaji na mtazamo wa wateja.**

**Hadi mwishoni mwa 2024, benki za Kiislamu zilikuwa zinashikilia karibu asilimia nane tu ya mali zote za sekta ya benki, kiwango kinachoonekana kuwa kidogo kwa nchi yenye Waislamu wengi.**

**Akifafanua changamoto hizo, profesa alisema kuna uelewa mdogo wa umma kuhusu bidhaa na faida za benki za Kiislamu na kwamba Waislamu wengi bado hawana taarifa za kutosha kuhusu tofauti kati ya mifumo ya Kiislamu na ile ya kawaida, huku baadhi wakiamini kuwa huduma za Sharia hazina ushindani wa kutosha au ni ghali zaidi.**

**Changamoto nyingine ni udogo wa taasisi nyingi za Kiislamu, hali inayozuia uwezo wao wa kupanua huduma, kuwekeza katika teknolojia ya kisasa na kushindana na benki kubwa za kawaida.**

**Ripoti iliyochapishwa na CNBC Indonesia inaeleza kuwa mtazamo wa muda mrefu wa ukuaji wa taratibu pia unatokana na elimu ya kifedha isiyo sawa kati ya maeneo ya mijini na vijijini, pamoja na upatikanaji mdogo wa huduma za kidijitali katika baadhi ya maeneo.**

## Mjadala waibuka Ghana ujenzi mpya chapa ya Benki ya Kiislamu bila kutaja Uislamu

**Juhudi za Benki Kuu ya Ghana kuanzisha kile kinachoitwa Mfumo wa Benki bila Riba (Non-Interest Banking - NIB) zimeibua mjadala mpana kuhusu mustakabali wa huduma za kifedha zinazofuata misingi ya Kiislamu nchini Ghana.**

**Hatua hiyo inalenga kupanua ujumuishaji wa kifedha bila kuibua mijadala ya kidini, lakini wachambuzi wanaonya kuwa mkakati huo unaweza kuleta matatizo makubwa ya kisheria na kiudhibiti.**

**Kwa mujibu wa mchambuzi wa sera Bright Simons, jaribio la kuondoa utambulisho wa kidini kwa kubadili jina kutoka Islamic Banking hadi Non-Interest Banking limezalisha kile anachokiita "utambulisho wa pande mbili."**

**Kwa upande mmoja, mwongozo wa BoG unakataza matumizi ya alama au majina yenye mnasaba wa kidini; kwa upande mwingine, unazitaka taasisi za NIB kufuata viwango vya kimataifa vya Accounting and Auditing Organization for Islamic Financial Institutions (AAOIFI), ambavyo vina mizizi ya wazi ya Kiislamu.**

**Mgongano huu, wachambuzi wanasema, si wa maneno tu bali ni wa kisheria. Benki zisizo na riba zinategemea dhana za fiqhi ya Kiislamu kama Mudarabah (ushirikiano wa faida), Murabahah (uuzaji kwa faida iliyokubaliwa) na Ijarah (ukodishaji). Dhana hizi hazina msingi wa moja kwa moja katika sheria ya kawaida ya Kiingereza au sheria za Ghana. Endapo migogoro itafikishwa mahakamani, majaji wanaweza kujikuta wakilazimika kuchagua kati ya sheria za kitaifa au viwango vya kidini, jambo linaloweza kuvuruga uhalali wa mikataba.**




MAKALA MAALUM

Na Wwandishi wetu
0787 503 085

## KENYA SIO KIGEZO CHA KILA TAIFA:

# Majibu kwa ulinganisho usiozingatia muktadha

Hoja kwamba kanisa nchini Kenya hukosoa serikali bila kuitwa udini au ukabila, ilhali hali kama hiyo Tanzania hutazamwa tofauti iliyotolewa na msomi mmoja hivi karibni inaonekana kuvutia juu juu.

Hata hivyo, hoja hii inajengwa juu ya ulinganisho dhaifu mno unaopuuzia historia, muundo wa jamii, na falsafa tofauti za ujenzi wa taifa katika nchi mbili hizi.

Mosi, ni upotoshaji wa wazi kudai kwamba nchini Kenya ukosoaji wa kanisa haujawahi kutafsiriwa kama siasa za utambulisho (udini). Historia ya Kenya imejaa mifano ambapo dini, kabila na siasa zimeingiliana kwa njia iliyoacha majeraha makubwa ya kijamii.

Kwamba, leo baadhi ya kauli za kanisa hupokelewa kama ukosoaji wa kawaida wa serikali hakumaanishi kuwa Kenya imepata mwarubaini au suluhisho la kudumu dhidi ya siasa za mgawanyiko; bali inaonesha uvumilivu uliolipiwa gharama kubwa.

Pili, hoja kwamba "hakuna mtu Kenya anayesema haya ni udini" si kweli na wala si sahihi kimsingi. Kauli za kanisa, hasa unapokaribia uchaguzi, mara nyingi huchambuliwa kwa mizani ya kikanda, kikabila na hata kimadhehebu. Tofauti ni kwamba Kenya imeuzoea mjadala huu au inajitia kuuzoea mjadala huo, si kwamba hauna hatari kwao.

Mtu anayeonekana mbele ya kadamnasi msomi anapodai kuwa eti wanasiasa "wa huku" hutumia hoja ya udini kama mbinu ya gawa uwatawale, anapuuza ukweli muhimu: Tanzania ilijengwa juu ya msingi wa makubaliano ya kimya kimya kwamba dini hazitakuwa chombo cha ushindani wa kisiasa. Huu haukuwa ujanja wa kisiasa bali ulikuwa mkakati wa makusudi wa kujilinda na kulizuia taifa changa kama hili kugawanyika na kusambaratika mapema.

Kwa kulinganisha, Kenya iliruhusu taasisi za dini kukua kama wahusika wakuu wa siasa za umma, hasa wakati wa mapambano ya kurejesha demokrasia ya vyama vingi. Hili lilikuwa chaguo lao la kihistoria — si kielelezo cha juu cha ustaarabu wa kisiasa.

Hoja kwamba Masheikh hawana nafasi katika kauli hizi za kisiasa nchini Kenya pia ni ya kupotosha. Ukweli ni kwamba uwakilishi wa sauti za kidini Kenya hauko sawa, na hii inaendana na mizania ya idadi ya waumini wa dini kuu.

Hali hii ikihamishiwa Tanzania bila tahadhari ingeibua maswali halali ya usawa wa kidini, uhalali wa kisiasa na uwakilishi sawia kwenye vyombo vya maamuzi.

Muhimu zaidi, hoja nzima ya mwandishi inaangukia pua kwa kosa moja la msingi: kudhani kuwa kile kinachofanya kazi Kenya kinapaswa kufanya kazi Tanzania. Huu ni upofu na mtazamo finyu unaopuuza ukweli kwamba uthabiti wa kisiasa haupimwi kwa kukosa adabu, ufedhuli, propaganda chafu na kelele za ukosoaji bali kwa uwezo wa jamii kubaki pamoja licha ya matatizo madogo madogo au tofauti zake.

Ndiyo maana, wakati mwingine wanasiasa hujificha nyuma ya pazia ya kauli za "umoja wa kitaifa" ili kuepuka uwajibikaji kama ngao; hasa pale wanapokosolewa kuhusu utendaji duni, rushwa, au kushindwa kutimiza ahadi, wanaweza kugeuza mjadala na kudai kuwa wakosoaji wao "wanahatarisha umoja wa taifa."

Kwa hapa, dhana ya umoja inatumika vibaya si kwa nia ya kulinda taifa, bali kuepuka uwajibikaji wa kisiasa. Lakini ni upungufu wa hoja kudai kuwa kila tahadhari dhidi ya siasa za kidini ni njama. Baadhi ya tahadhari hizo zimetokana na hofu halisi ya kuepuka kuiyumbisha misingi ya mshikamano wa taifa.

Kwa hiyo, kabla ya kuisifu Kenya kama mfano wa kuigwa, ni busara kukubali ukweli huu: Kenya imechagua kuishi na hatari za siasa za utambulisho (udini na ukabila); Tanzania imechagua kuzipunguza mapema.

Njia hizi mbili zina gharama na faida zake. Lakini kuzilinganisha bila muktadha ni uchambuzi dhaifu unaovaa kizubao cha usomi. Tafakari ya kina inatufundisha kuwa demokrasia haina sura moja, na hekima ya kisiasa iko katika kuelewa muktadha kabla ya kutoa hukumu.

### Mwito na tafakari ya kina:

Badala ya kuiga mifumo ya majirani zetu bila tafakari, ni wajibu wa wasomi na wachambuzi wetu wa siasa kujiuliza swali hili gumu: ni nini hasa kililifanya taifa laTanzania lidumu kwa amani na mshikamano kwa muda mrefu?

Afya
Pure Drinking water
"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.
WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com


رجب

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

# Wajibu wa Waislamu kuikomboa Palestina!



Palestina ni ardhi tukufu ya Kiislamu, ambayo Umar al–Farooq (Allah amridhie) aliifungua, Salahuddin al–Ayyubi akaikomboa, na Khalifah Abdul–Hamid akailinda. Ardhi ya Palestina haiuzwi na haikubaliki watu wake kugawanywa na yule anayeikalia kimabavu, ambaye amekuwa akiwafukuza watu wake kutoka kwenye ardhi hii.

Ufumbuzi wa mgogoro wa Palestina na Israel, ambayo inaikalia kimabavu, siyo kuundwa kwa Dola ya Palestina sambamba na Israel katika ardhi hii ya Waislamu (Two State Solution), kama inavyopendekezwa na Mabeberu wa Magharibi.

Badala yake, ufumbuzi wa kweli wa mgogoro huu ni kama alivyosema Allah 'Azza Wajallah' ndani ya Qur'an Tukufu, akiwaambia Waislamu pale wanapovamiwa na kufurushwa na maadui kwenye ardhi zao. "Na piganeni katika Njia ya Allah na wale wanaokupigeni, wala msianze uadui. Kwani Allah hawapendi waanzao uadui. Na waueni popote muwakutapo, na muwatoe popote walipokutoeni; kwani fitina ni mbaya zaidi kuliko kuua..." [Qur'an, 2:190–191].

Wajibu wa juu kabisa wa sharia unaozidi mwingine wote ni kuwasaidia wanyonge na kuikomboa ardhi inayokaliwa kimabavu. Wajibu huu unaangukia si tu kwa wananchi, bali kimsingi kwa nchi za Waislamu zilizoshika dola na majeshi yenye silaha na nguvu za kupambana. Ni juu ya mabega yao kwamba wajibu mkubwa wa Jihad katika njia ya Mwenyezi Mungu umelala. Imam Nawawi (Allah amrehemu) amesema: "Ikiwa makafiri wamevamia ardhi ya Waislamu au kuuzingira mji, basi Jihad inakuwa wajibu wa mtu binafsi (fardh ayn) kwa wale walio karibu zaidi, na kisha wale wanaofuatia kwa ukaribu."

Kadhalika, Imam Qurtubi (Allah amrehemu) amesema: "Wakati Jihad inapokuwa wajibu wa mtu binafsi, hairuhusiwi kwa yeyote kubaki nyuma, labda awe na udhuru wa wazi unaokubalika kisheria. Yeyote anayefanya hivyo anatenda dhambi kubwa."

Nae Ibn Qudama amesema: "Iwapo adui ananyemelea ardhi au Imam anatoa wito kwa watu kushika silaha, basi hiyo inakuwa faradhi kwa kila mmoja kutoka, na hairuhusiwi kwa yeyote kubaki nyuma."

Ndugu zangu katika imani, mauaji ya kimbari yanayoendelea Gaza siyo janga la mbali, bali ni mstari wa mbele wa harakati za umma wetu kupinga dhuluma katika ardhi hii tukufu. Kaka na dada zetu wa Palestina hawapiganii madaraka au utajiri wa hapa duniani.

Wao wamesimama kama walinzi, wakijitolea maisha yao kwa ajili ya kunusuru kila inchi ya ardhi hii, ambayo ni mali ya Waislamu, wakilinda utukufu wa umma wetu dhidi ya mashambulizi ya makafiri wapenda vita.

Nukta ya msingi hapa ni kwamba, Waislamu lazima wakumbuke kuwa ufumbuzi wa dola mbili (Two State Solution) unaopigiwa debe na mataifa ya Magharibi, maana yake ni kuyatambua rasmi madai potofu ya Mazayuni kwa ardhi hii tukufu ya Waislamu. Jambo hili limekatazwa katika sharia.

Masahaba watukufu na mujahidina waadilifu wamemwaga damu zao pale. Isitoshe, Palestina ni eneo la msikiti wa tatu kwa utukufu, lakini pia ni eneo la Hijja kwa Waislamu wa ulimwengu mzima. Ni mahali ambapo safari ya Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) kwenda Mi'iraji ilifanyika, na ni qibla cha kwanza cha Waislamu kabla ya Makka.

Kwa hiyo, Palestina ni ardhi ambayo Waislamu hawapaswi kuiachia hata inchi yake moja kwa maadui. "Piganeni nao, Mwenyezi Mungu atawaadhibu kwa mikono yenu, na atawaaibisha na atawasaidia kuwashinda, na atavipoza vifua vya Waumini." [Qur'an, 9:14].

رَجَب

**MAKALA MAALUM**

0712 690 811

NA SHEIKH SEIF RUGA



# Madhara makubwa ya kamari kidini na kidunia

**Miongoni mwa rehema za Allah kwa waja wake ni kuwaridhia dini ya Uislamu kuwa sharia yao – dini iliyoleta kila jambo lenye manufaa kwa binadamu katika maisha ya dunia na Akhera. Allah Mtukufu anasema: "Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na nimetimizia neema Yangu juu yenu, na nimeridhia Uislamu uwe ndiyo Dini yenu." [Qur'an, 5:3].**

Mafundisho ya Uislamu aliyoyaweka Allah hayahusiani na ibada za kiroho tu, bali pia mambo yanayohusu maisha yote ya mwanadamu hapa duniani, ikiwamo miamala baina ya mtu na mwenzake, na baina ya mtu na Mola wake.

Ukizitafakari sharia hizi za mbinguni, utakuta kuwa zimekusanya maslahi yote ya wanadamu na sababu za ustawi wao. Wanaoshikamana nazo kikamilifu hupata ushindi, nguvu na utukufu. Lakini wanaozipuuza na kuzembea katika kuzitekeleza au kuacha baadhi yake hupata unyonge, udhalili na mateso ya maadui zao; na hii ndiyo kanuni ya Allah ya kimaumbile kwa viumbe wake.

Wanafalsafa husema: "Haifai kulitolea hukumu jambo lolote ila baada ya kulifahamu." Wanazuoni wa mwanzo na wa sasa wa Kiislamu wameilezea kamari kwa matamshi tofauti lakini yenye maaana moja.


Mwanazuoni Az–Zuhr (Allah amrehemu) ameilezea kamari kuwa ni kutupa mishale ya bahati nasibu juu ya mali au mazao. Nae mwanazuoni wa zama hizi, Sheikh Dkt. Yusuf al–Qardhawi (Allah amrehemu) ameilezea kamari kuwa ni kila mchezo ambao mshiriki haepuki moja ya mambo mawili; kupata faida au hasara.

Katika nyakati za leo, aina za kamari zimeongezeka sana kwa sababu ya maendeleo ya teknolojia, vyombo vya habari na mtandao wa intaneti. Miongoni mwa aina hizo ni kubashiri michezo ya soka na mashindano mbalimbali, kubeti kupitia ujumbe mfupi wa simu, na kwenye runinga na redio kwa kutuma gharama za kushiriki.

Ingawa hupewa majina mazuri na ya kuvutia, kama vile zawadi, bahati nasibu, mchongo au mkwanja – majina hayo hayabadilishi uhalisia wake kuwa kamari ni haramu. Allah Mtukufu anasema: "Wanakuuliza (Muhammad) kuhusu pombe na kamari. Sema: Katika vyote viwili kuna madhara makubwa...." [Qur'an, 2:219).

Kadhalika, Allah Mtukufu anasema: "Enyi mliyoamini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo ili mpate kufanikiwa. Hakika shetani anataka kutia kati yenu uadui na chuki kwa ulevi na kamari, na akuzuieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusali. Basi je, mmeacha?" [Qur'an, 5:90–91].

Kwa hivyo, pombe na kamari vina madhara makubwa ambayo Uislamu ulikuwa wa kwanza kupambana nayo ili kulinda familia, jamii na taifa zima. Fedha au mali inayopatikana kwa njia ya kamari ni haramu na haiwezi kukubaliwa na Allah kama sadaka, zaka, au hata kujenga misikiti au kuitoa wakfu.




Hata dua ya mtu anayecheza kamari haikubaliwi na Allah Mtukufu, kwa ushahidi wa kauli ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) aliposema: "Hakika Allah ni mwema na hakubali ila kilicho chema tu." [Muslim].

Kama ambavyo kamari ina madhara yanayohusiana na dini na humuweka mhusika kwenye hatari ya kupata ghadhabu ya Allah na adhabu ya Siku ya Kiyama, vivyo hivyo ina madhara mengine yanayohusiana na maisha ya dunia, ambayo huharibu utulivu na kuondoa ladha ya maisha.

Baadhi ya madhara hayo yametajwa katika Qur'an, na mengine yanaonekana wazi katika maisha ya kila siku ya wanaojishughulisha na michezo ya kamari. Kamari husababisha uadui na chuki kati ya watu wanaocheza kamari kwa aina zake zote, lakini pia inachangia kuenea kwa uhalifu kama vile wizi na udokozi.

Anayetazama mchezo wa kamari huona jinsi mtu mmoja anavyopoteza mali yake kwa haraka na mwingine kupata kwa sekunde chache, hivyo humvutia na kumpa tamaa ya kujaribu. Mara nyingi mtu mwenye tabia ya kucheza kamari hutumia njia haramu kama wizi ili kuridhisha hamu yake.

Kamari husababisha mauaji, na mara nyingine mchezaji huchukizwa na kupotea kwa mali aliyohangaika kuipata kwa muda mrefu. Hasira zinapomzidi anaweza kujidhuru mwenyewe (kujiua) au kumuua mwenzake kwa lengo la kurejesha kile alichopoteza. Haya ndiyo matokeo ya kawaida ya wale wanaoshinda na wanaoshindwa katika kamari.

Kwa sababu hii, sehemu nyingi za kuchezea kamari huwa ni maskani ya ufuska, ulevi, dawa za kulevya na maovu mengine. Kamari imeharibu maisha ya familia nyingi baada ya kuishi katika neema kwa miaka mingi, imesababisha familia hizo kutawanyika na watoto kuwa mitaani bila msaada wala uangalizi.

Kamari ni njia ya mapato yasiyokuwa halali, kwani msingi wake ni bahati tu na si kazi wala jitihada. Hivyo kamari haizai manufaa yoyote kwa jamii isipokuwa hasara, umasikini na vurugu. Mtu anapozama kwenye michezo ya kamari hupoteza utulivu wa akili na hisia, na haoni madhara ya pesa zinazotoweka mikononi mwake. Anakubali apoteze chochote alichonacho kwa tamaa ya kutaka kupata kingi zaidi.

رجب

NASAHA ZA WIKI

0787 503 085

NA YUSUFU AMINI



# Uislamu utapiga hatua kwa mambo haya sita

**Katika makala haya, leo nataka tuangalie kwa ufupi mambo sita ambayo iwapo Waislamu wakishikamana nayo watapiga hatua kubwa za maendeleo ya kidini na dunia pia. Mambo hayo sita ambayo yamefafanuliwa vyema katika Qur'an tukufu, Sunna za Mtume (rehema za Allah na amani imshukie), na kupitia matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa na wasomi wa Kiislamu; ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya dini na watu wake. Mambo hayo ni pamoja na elimu, umoja, takwimu sahihi, uchumi imara, uongozi adili na vyombo vya habari.**

## Tuanze na elimu

Elimu ndiyo nyenzo inayompatia mwanadamu maarifa ya kumwezesha kufanya kazi kwa kutumia rasilimali zinazomzunguka. Kwa hiyo, twaona kuwa elimu ni ufunguo, hazina, ngao, silaha, mwanga, hifadhi, ushindi na ukombozi.

Lakini ieleweke hapa kwamba, vyovyote itakavyokuwa, elimu haiwezi kuwa na manufaa ikiwa haimuwezeshi mtu kuyakabili na kuyatawala mazingira yake (ukhalifa) wala kupata radhi za Mola wake (uongofu).

Nafasi na umuhimu wa elimu vimebainishwa tangu pale Mtume Muhammad (rehema za Allah na amani imshukie) alipopewa Utume. Haifai kutenganisha kati ya elimu ya muongozo (dini) na mazingira kwani zote hushirikiana kumuwezesha binadamu kufikia lengo moja la kutafuta fadhila na radhi za Mola.

Ili tuweze kupiga hatua na kufanikiwa, ni lazima tujizatiti katika suala la elimu kwa kuweka mikakati madhubuti kuanzia ngazi ya msikiti hadi taifa katika mnyambuliko maalumu. Kwenye msikiti kuwe na maktaba, vitabu, majarida na magazeti; kwenye mtaa au kijiji kuwe na madrasa na chekechea ya Kiislamu.

Katika kata iwepo shule ya msingi ya Kiislamu; kwenye tarafa kiwepo chuo cha ufundi cha Kiislamu; na katika wilaya kuwe na shule ya Sekondari ya Kiislamu. Mkoani kuwe na shule ya sekondari ya juu ya Kiislamu (kidato cha tano na sita) sambamba na chuo cha Kiislamu cha ualimu kwa kiwango cha cheti na astashahada; na katika ngazi ya kanda au taifa kiwepo Chuo Kikuu cha Kiislamu.

## Umoja

Aidha, katika safari ya kuyasaka mafanikio, ni lazima tuepuke mizozo inayotokana na ikhtilafu za kifiqhi, mfano katika suala la kufunga mikono kwenye sala. Ikhtilafu za namna hii hazipaswi kuwafanya Waislamu wasali misikiti tofauti.

Qur'an yatuambia: "Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake wala msizozane msije mkaharibikiwa na kupoteza nguvu zenu, na subirini (vumilianeni). Hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiei." [Qur'an, 8:46]. Kwa hiyo, ikitokea ikhtilafu yoyote baina yetu tunatakiwa kuvumiliana na kumuachia Allah ahukumu.

Ni ujahili wa hali ya juu kumbagua Muislamu mwenzio kwa sababu ya tofauti za kimadhehebu. Tunapaswa kuliepuka hili kwa sababu, kubaguana kwa misingi ya ikhtilafu ni kuwaruhusu maadui wavuruge umoja wetu wa kidini.

## Takwimu sahihi

Takwimu sahihi ndiyo msingi mkubwa wa mipango, utekelezaji na tathmini ya maendeleo ya jamii yoyote ile. Hivyo, jamii ya Kiislamu inatakiwa kuwa na takwimu sahihi ili kuweza kusimamisha Uislamu nchini na duniani kote, pamoja na kutathmini hali ya Uislamu kwa siku zijazo.

## Uchumi imara

Uislamu hauwezi kusimama bila uchumi imara, kwa kuwa mali imepewa nafasi ya kwanza baada ya imani katika kupigania na kusimamisha dini ya Uislamu. Katika kulifikia hili, tunatakiwa kuwa na njia tatu madhubuti za kufikia uchumi imara wa Waislamu katika nchi yoyote ile.

Njia hizo ni kufanya kazi kwa bidii, kutoa katika vile alivyoturuzuku Allah – yaani mali, nafsi, maarifa, hekima, nguvu, muda, ushawishi, pamoja na kuacha yanayobakia katika riba na kamari.

## Uongozi adili

Hatuwezi kuishi vizuri bila uongozi. Hata hivyo, kinachotakiwa si bora uongozi bali uongozi bora unaotokana na Waislamu wa kweli na ambao wanakubalika kwa Waislamu walio wengi, ili hatimae uongozi wao uwe ni mwamvuli wa kila anayejitambua kuwa ni Muislamu.

Tatizo kubwa lililopo sasa ni jinsi gani anapatikana kiongozi wa Waislamu. Allah na Mtume wake wamekwishaeleza jinsi ya kupata viongozi bora, lakini changamoto inakuja pale watu wanaposimika viongozi kwa maslahi yao binafsi ya kidunia.

## Vyombo vya habari

Umuhimu wa Waislamu kuwa na vyombo vya habari ni kuwa, viwatumie wanazuoni wachache waliopo kuufikishia ulimwengu mzima taarifa sahihi kuhusu Allah Mtukufu na Mtume wake (rehema za Allah na amani imshukie), pamoja na habari sahihi zinazohusu dini na dunia.

Waislamu wana dhima na wajibu wa kufuatilia kwa karibu vyombo vya habari vilivyopo hata kama si vya Waislamu ili kujua yale yanayoendelea ulimwenguni.

رَجَب

SEHEMU YA 2

MUSSA IMANI
SHEHA,
ZANZIBAR
0773 181 494



# VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

# USAMA BIN ZAID

## Kipenzi cha Mtume na mtoto wa kipenzi cha Mtume

**Katika toleo lililopita, tulianza kujifunza jina kamili na nasabu ya Usama, tarehe na mahala alipozaliwa, wasifu na ukaribu wake na Mtume (Allah amshushie rehema na amani). Pia, tulianza kuzungumzia mchango wake katika harakati za mapambano dhidi ya maadui wa Uislamu. Wiki hii tunaendelea kuelezea maeneo mengine ya ushiriki wake huo, endelea...**

### Usama ateuliwa kuliongoza jeshi

Mwanzoni mwa mwaka wa 11, Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliamrisha kuandaliwa jeshi kubwa kwenda kuwapiga Warumi. Katika jeshi hilo, palikuwa na idadi kubwa ya wakuu wa Maswahaba wakiwemo: Abubakr, Umar, Sa'd bin Abi Waqqas, Abu Ubaeida na wengineo. Licha ya uwepo wa vigogo hao, alimchagua Usama kuwa kiongozi wao licha ya udogo wa umri wake (miaka 20).

Jeshi likiwa katika maandalizi, mara zikaja taarifa za kuzidi maradhi ya Mtume, likajizuia kutoka na kupiga kambi nje kidogo ya Madina. Usama anaeleza: "Ugonjwa ulipomzidia Mtume, nilitoka mimi na watu wengine kumuona na tulimkuta hawezi tena hata kusema. Akawa anaashiria tu kwa mkono wake, akiupeleka juu chini, nikaelewa kwamba alikuwa akiniombea dua." Hapakupita muda mwingi, mara Mtume (rehema na amani zimshukie) akafariki dunia na akachaguliwa Abubakr kuwa Khalifa.

### Abubakr apeleka Jeshi la Usama

Moja ya mambo muhimu aliyoyatekeleza Khalifa Abubakr (Allah amridhie) lilikuwa ni kuliruhusu jeshi la Usama. Lakini baadhi ya Maswahaba (Ma'answar) hawakuafiki hatua hiyo.

Hao ambao hawakuafiki, walikuwa na maoni kinyume. Walimuomba Umar (Allah amridhie) amshauri Khalifa asifanye haraka kumpeleka Usama, na ni vyema amchaguwe kiongozi ambaye anampita Usama kiumri.

Umar alipofika kwa Khalifa na kuanza kuwasilisha ujumbe wa Answar, Khalifa alimkamata ndevu na kuyadakiza – huku akiwa amekasirika- na kumwambia: "Yaani amechaguliwa na Mtume wewe unanitaka niuondowe uongozi kwake!? Wallah hilo haliwezekani!"

Aliporudi kwa waliotoa maoni wakamuuliza alichosema Khalifa aliwajibu: "Tekelezeni agizo la Khalifa. Yaliyonifika mbele ya Khalifa wa Mtume kwa sababu yenu –kwa kweli- ni makubwa." [Taz. Suwarun min hayat swahaba uk 230].

### Khalifa Abubakr alisindikiza jeshi

Jeshi lilipoondoka chini ya uongozi wa kijana Usama bin Zaid (Allah amridhie), Khalifa alililisindikiza huku akitembea kwa miguu, na Usama akiwa amepanda mnyama.

Usama akamwambia Khalifa: "Panda wewe." Akasema: "Hapana." Usama akamwambia: "Wallahi utapamnda au nitashuka na mimi nitembee kwa miguu." Akamjibu: "Wallah hutoshuka na mimi sipandi, kwani kuna tatizo gani kuzichafua nyayo zangu kidogo kwa ajili ya dini ya Allah?"

Baada ya hapo, Khalifa Abubakr alimuombea dua na kumtaka atekeleze maagizo ya Mtume, kisha akamwambia: "Kama utaona ni sawa kuniachia Umar (Madina) utanisaidia sana." Usama akamuidhinisha Umar kubaki Madina kwa ombi la Khalifa, amsaidie katika kusimamia majukumu ya kiuongozi.

Itaendelea inshaAllah.

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Bunduki zatajwa janga la afya ya umma kwa Wamarekani Weusi



Uhuru mkubwa wa mauzo ya bunduki nchini Marekani umejengeka kwa muda mrefu chini ya hoja ya usalama binafsi na haki ya kikatiba. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni — hususan wakati wa janga la UVIKO-19 — uhuru huo umegeuka kuwa chanzo kikuu cha janga la afya ya umma, hasa katika jamii za watu weusi.

Badala ya kuleta usalama, upatikanaji holela wa silaha umeongeza vifo, majeraha ya kudumu, msongo wa mawazo na mzunguko wa hofu unaojirudia kizazi hadi kizazi.

Takwimu za afya ya umma zinaonyesha pengo kubwa la athari za bunduki kwa misingi ya rangi. Watu weusi, hasa wanaume na wavulana, wamekuwa wahanga wakubwa wa mauaji kwa bunduki kuliko makundi mengine.

Ingawa ni asilimia ndogo ya idadi ya watu, wanachangia zaidi ya nusu ya wahanga wa mauaji. Hii ina maana kuwa bunduki si tu tatizo la uhalifu, bali ni tatizo la kiafya linaloathiri jamii fulani kwa uzito usio sawia.

Sekta ya silaha imeongeza uzalishaji na mikakati ya mauzo, ikibadilisha hadhira yake kutoka wateja wa jadi kwenda kwa jamii za watu weusi na makundi mengine yaliyo hatarini. Ujumbe unaotumika mara nyingi huchezea hofu: uhalifu, maandamano, ukosefu wa uaminifu kwa vyombo vya dola, na sintofahamu za kisiasa.

Bunduki huuzwa kama "kinga binafsi," ilhali tafiti zinaonyesha kuwa umiliki wa bunduki huongeza hatari ya kuuawa au kujiua ndani ya nyumba. Kwa maneno mengine, bidhaa inayodaiwa kulinda maisha mara nyingi huyaweka hatarini zaidi.

Wakati wa janga la UVIKO-19, serikali ya shirikisho ilitangaza maduka ya bunduki kuwa biashara muhimu, huku sekta hiyo ikipata misaada ya kifedha ya mamilioni ya dola. Wakati huo huo, ukaguzi na udhibiti wa mauzo ulilegea. Matokeo yake yalikuwa ongezeko kubwa la mauzo ya bunduki, wakiwemo wanunuzi wa mara ya kwanza.

Ndani ya muda mfupi, silaha nyingi zaidi zilianza kuonekana katika matukio ya uhalifu na vyumba vya dharura, na idadi ya vifo kwa bunduki ikavunja rekodi.

Athari za bunduki haziishii kwenye vifo. Maelfu ya watu hubaki na ulemavu wa kudumu, maumivu sugu na kiwewe cha kisaikolojia (PTSD).

Familia hubeba mzigo wa huzuni, hofu na gharama za matibabu. Jamii zilizoathirika hupoteza vijana wenye ndoto na uwezo, na kuingia kwenye mzunguko wa kiuchumi na kijamii unaodhoofika. Haya yote ni dalili za janga la afya — si tukio la uhalifu pekee.

Kinachoongeza tatizo ni ukosefu wa udhibiti wa afya na usalama kwa bidhaa za bunduki. Tofauti na bidhaa nyingine za watumiaji, bunduki hazifungwi na viwango madhubuti vya afya ya umma katika ngazi ya kitaifa.

Mamlaka zinazopaswa kulinda walaji dhidi ya matangazo ya kupotosha mara nyingi hazichukui hatua, hata panapodaiwa kuwa silaha "huzuia uhalifu" bila ushahidi wa kisayansi. Pengo hili la udhibiti huruhusu masoko yanayochochea hofu kuendelea bila uwajibikaji.

Ni kweli kwamba baadhi ya watu weusi huona umiliki wa bunduki kama njia ya kujilinda katika mazingira yenye uhalifu na historia ya kutokuaminiana na vyombo vya dola. Mtazamo huu una mizizi ya kihistoria na kijamii.

Hata hivyo, suluhisho la kiafya la muda mrefu halipo katika kuongeza silaha, bali katika kupunguza sababu za hofu: umaskini, ukosefu wa fursa, makazi duni, huduma haba za afya ya akili, na mifumo ya haki inayokosa uaminifu wa jamii.

Kukabiliana na janga hili kunahitaji mabadiliko ya sera na mtazamo. Udhibiti makini wa mauzo na matangazo, uwekezaji katika huduma za afya ya akili, uzuiaji wa vurugu unaoongozwa na jamii, na uwajibikaji wa sekta ya silaha ni hatua muhimu.

Zaidi ya yote, mjadala wa bunduki unapaswa kurejeshwa kwenye kiini chake: kulinda uhai na afya ya binadamu, hasa kwa jamii ambazo kwa muda mrefu zimebeba mzigo mkubwa wa maumivu.

Kwa kuangalia bunduki kama suala la afya ya umma — na si ishara ya uhuru au kinga binafsi pekee — Marekani inaweza kuanza kupunguza majeraha na vifo vinavyoathiri jamii za watu weusi.

Bila mabadiliko hayo, uholela wa mauzo ya bunduki utaendelea kulisha janga la afya linaloangamiza maisha, familia na mustakabali wa vizazi vijavyo.


Sikiliza Radio
Imaan FM
Dar es Salaam
104.5fm
Arusha 90.8fm
Mwanza 106.5fm
Mbeya 90.3fm
Tabora 101.6fm
Ruvuma 94.2fm
Mtwara 90.9fm
Kigoma 92.5fm
/radioimaanfm
MOROGORO
96.3 fm
MSAMVU
Elimu Bila Mipaka

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA




# Vijana wahamasishwe kujipamba na Uislamu

Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Hatoingia Peponi mwenye chembe ya kiburi moyoni mwake." Mtu mmoja akauliza: "Hakika mtu hupenda nguo yake iwe nzuri na viatu vyake viwe vizuri." Mtume akasema: "Hakika Allah ni Mzuri na anapenda uzuri. Kiburi ni kukataa haki na kuwadharau watu." ***[Muslim].***

## Mafundisho ya tukio

Uislamu umehalalisha na kuhimiza watu kujiweka katika muonekano mzuri bila kupindukia mipaka iliyowekwa kisheria. Vilevile, Uislamu una ishara na alama zake zinazoonekana wazi kwa Muislamu, ambaye ukikutana naye ni rahisi kupata fadhila kupitia yeye kwa kumtolea salamu kutokana muonekano wake unaoashiria kuwa yeye ni Muislamu.

Mtume (rehema na amani zimshukie) alieleza mambo kumi ya fitra (maumbile), na miongoni mwa hayo ni kupunguza masharubu, kufuga ndevu, kupiga mswaki, kukata kucha, na kuondoa nywele za kwapa na za sehemu za siri. Yote haya yanahusiana na usafi wa mwonekano.

Aidha, miongoni mwa sharia zinazoonesha uhusiano wa dhahiri ya mtu na ndani yake ni hijab ya mwanamke Muislamu. Allah ameamuru wanawake wajisitiri na amewakataza kuonesha mapambo yao, huku akibainisha sababu ya kuwaamrisha kuwa ni usafi wa nyoyo za wanaume na wanawake: "Na mnapowaomba (wanawake) kitu, waombeni nyuma ya pazia, hilo ni takaso zaidi kwa nyoyo zenu na nyoyo zao." [Qur'an, 33:53].

Kwa minajili hiyo, utaona kuwa hijab ni sitara ya kisheria kwa mwanamke, vilevile ni pambo linaloonesha Uislamu wake kwa dhahiri.

## Hali ya watu wengi hivi sasa

Ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya Waislamu wanahisi aibu au uzito kujiweka katika muonekanao wa Kiislamu. Hali hii huashiria kasoro kubwa katika nyoyo za watu hawa.

Hakika ampendae Allah na kuridhia amri zake hufurahia kuzitekeleza kwa haraka na kwa fahari kubwa, kama walivyofanya wanawake wa Answari wakati ilipoteremka amri ya hijab. Bila kusita, haraka sana wanawake wale walichana mashuka yao na kujisitiri.

## Kujitofautisha na makafiri

Uislamu, pia umehimiza kujitofautisha na wasiyokuwa Waislamu katika muonekano wa nje, mfano kwenye suala la kupaka rangi nywele au ndevu zenye mvi. Uislamu unaruhusu kuzibadili nywele au ndevu zenye mvi kwa kuzipaka rangi iliyo na mchanganyiko wa nyeusi na nyekundu, hina, au kwa shakili ya manjano.

Hizi ni katika alama za Uislamu ambazo Masahaba na wengineo katika wema waliopita walizidhihirisha katika vitendo vyao vya wazi. Kuzibadili nywele au ndevu zenye mvi kwa kuzipaka rangi ni katika mambo ambayo watu wa Kitabu (Mayahudi na Manasara) wanajizuilia wakidhani kuwa kujipamba huko ni kinyume na uchamungu, kama wafanyavyo watawa wao.

Waislamu wa Ahlus Sunnat Wal–jama'a wanaamini kuwa imani ni kusadikisha kwa moyo, kauli ya ulimi na matendo ya viungo. Muonekano wa nje ni dalili ya yaliyomo ndani ya kiwiliwili. Ikiwa ndani kuna kheri, basi kheri hiyo lazima ionekane kwa nje; na ikiwa ni kinyume athari zake pia huonekana.

## Muonekano wa nje hautoshi

Watu wengi wanaegemea katika utekelezaji wa mambo ya wajibu wakidhani kuwa yanatosha, na wakati mwingine hujitetea kuwa muonekano wa nje si lolote kwa sababu hata wanafiki walionekana wakisali lakini walikuwa ni waongo.

Ni kweli kuwa hali ya wanafiki wakati wa Mtume (rehema na amani zimshukie) ni mfano wa wazi. Wao walihudhuria ibada ya sala msikitini kwa ria na unafiki, lakini sala haikuwazidishia kitu isipokuwa upotovu. Qur'an waliyoisikia haikuwazidishia chochoche ila upofu.

Allah anasema, nyoyo zao zilikuwa na maradhi, na kwa sababu hiyo vitendo vyao vilifichua maradhi hayo. Haikuwezekana kwao kuficha kabisa yaliyo nyoyoni mwao kwa sababu ni lazima yadhihirike. Muislamu anatakiwa aupende na kuudhihirisha Uislamu katika kila kipengele cha maisha yake ikiwa ni pamoja na muonekano wake.

Sharia ya Kiislamu imekuja kuwatofautisha Waislamu na watu wengine katika muonekano wao, mavazi yao na desturi zao. Anayetafakari mienendo ya baadhi ya vijana wetu wa leo ataona jambo hatari, nalo ni kupoteza muonekano wa Kiislamu kwenye maisha yao, hasa katika kunyoa ndevu na kupunguza masharubu.

Jambo hili linapingana na mwongozo wa Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie). Mtume ametuambia: "Kuweni kinyume na washirikina; fugeni ndevu kwa wingi na punguzeni masharubu." [Bukhari na Muslim]. Sheria ya Uislamu inakataza wanaume kujipamba kwa mitindo isiyofaa ya ndevu na nywele, kusuka nywele au kufuga/ kusokota rasta, kuvaa hereni na bangili, na kuvaa mavazi yenye chapa maarufu (brand) zinazowaunga mkono makafiri.

Aidha, sheria inakataza wanawake kutumia vipodozi vyenye kemikali na kuvaa hadharani mavazi laini yenye kuonesha maungo ya mwili. Yote haya ni mambo mabaya yaliyokatazwa katika dini. Katika hadith iliyonukuliwa na Bukahri, Mtume (rehema za Allah na amani zimshukie) amesema: "Allah amewalaani wanaume wanaojifananisha na wanawake, na wanawake wanaojifananisha na wanaume."

Inasikitisha kuona vijana wengi wa zama hizi wanaiga tabia na mienendo ya wanasoka, wanamuziki na wacheza filamu wa Kimagharibi, huku wakipuuza kabisa tabia za Kiislamu alizofundisha Mtume (rehema na amani zimshukie). Vijana wengi leo hii wameacha desturi nzuri za wazazi wao ambazo wamezirithi kutoka kwa babu zao, zilizopambwa na adabu za Kiislamu na kukubaliwa na wanazuoni na kufanyiwa kazi.

Kulinda desturi njema na mila nzuri za Kiislamu ni katika maslahi makubwa yaliyothibitishwa na Uislamu, kwa kuwa zinawatofautisha na watu wengine. Kwa kupoteza desturi njema na mila nzuri za Kiislamu, haiba na utu wa Muislamu huyeyuka katika mawimbi ya utandawazi.

IDARA YA DAAWA

## Mtume ﷺ amesema:

"Muislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wamesalimika kutokana na ulimi wake na mkono wake, na Muhajir (mhamaji wa kweli) ni yule anayeacha kile alichokataza Mwenyezi Mungu."

Bukhari

رَجَب

MAKALA
MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Fanya haya kukabiliana na changamoto za kitabia za mtoto



Wazazi wengi wanakabiliana na changamoto za kitabia za watoto katika hatua mbalimbali za ukuaji. Mtoto anapolia sana, kukasirika kupita kiasi, kukaidi maelekezo au kuonyesha ukaidi shuleni na nyumbani, hali hii huweza kuleta msongo mkubwa kwa mzazi na familia kwa ujumla.

Ingawa ni rahisi kuona tabia hizi kama ukaidi wa makusudi, mara nyingi huwa ni ishara ya changamoto za kihisia au kimaendeleo ambazo mtoto bado hajajifunza kuzimudu kikamilifu.

Watoto wengi huonyesha tabia ngumu kwa sababu bado wanajifunza stadi za msingi kama kujizuia, kudhibiti hasira, kutatua matatizo na kuwasiliana mahitaji yao kwa njia sahihi.

Katika mchakato huu wa ukuaji, kulipuka kwa hisia au kuvunja sheria huwa ni sehemu ya kujifunza. Hata hivyo, tabia hizi zinapozidi au kujirudia mara kwa mara, huanza kuathiri uhusiano kati ya mzazi na mtoto, na ndipo hatua za makusudi zinahitajika kuchukuliwa.

## Elewa chanzo cha tabia za mtoto

Ili kukabiliana na changamoto za kitabia, mzazi anapaswa kuanza kwa kuelewa chanzo cha tabia hizo. Wataalamu wa saikolojia ya watoto wanaeleza kuwa tantrums na hasira kali mara nyingi si za makusudi, bali ni tabia zilizojifunza.

Mtoto anapogundua kuwa kulia au kupiga kelele humletea anachotaka, huendelea kutumia njia hiyo kwa kukosa mbinu mbadala za kuwasiliana.

Zaidi ya hilo, tabia za mtoto zinaweza kuchochewa na njaa, uchovu, mabadiliko ya ghafla ya ratiba, au maelekezo yasiyo wazi.

Watoto wengine huonyesha tabia ngumu nyumbani lakini si shuleni, au kinyume chake, jambo linaloashiria kuwa mazingira na matarajio ya watu wazima yanachangia pakubwa. Kutambua mifumo hii huwasaidia wazazi kuzuia matatizo kabla hayajatokea.

## Usikate tamaa, usipaniki

Wazazi wengi huhisi kukata tamaa wanapojaribu mbinu mbalimbali bila mafanikio. Hata hivyo, uthabiti na utulivu ni nguzo kuu katika kudhibiti tabia za mtoto.

Kupiga kelele, kuadhibu kwa hasira au kutoa kile mtoto anachotaka wakati wa mlipuko wa hisia mara nyingi huimarisha tabia mbaya. Badala yake, mzazi anapaswa kubaki mtulivu na kuweka mipaka iliyo wazi na ya kudumu.

Ni muhimu pia kulenga tabia maalumu badala ya kumhukumu mtoto kwa ujumla. Tabia inayolengwa inapaswa kuwa wazi, inayoonekana na inayopimika.

Pongezi za wazi kwa tabia njema, kama "nimefurahi umeanza kazi ya shule kwa wakati," humsaidia mtoto kuelewa kinachotarajiwa. Adhabu au matokeo ya tabia mbaya yanapaswa kuwa ya haraka, yanayolingana na kosa, na kutekelezwa kwa uthabiti bila jazba.

## Zuia matatizo kabla hayajatokea

Mikakati ya kuzuia mara nyingi huwa na nguvu zaidi kuliko adhabu. Mzazi anaweza kurekebisha mazingira ili kumsaidia mtoto kudhibiti tabia zake. Kwa mfano, wakati wa kazi za shule, kuondoa vishawishi kama runinga au simu, kuhakikisha mtoto amekula na amepumzika, na kutoa mapumziko mafupi husaidia kupunguza msongo.

Mabadiliko ya shughuli, kama kuacha kucheza na kwenda kulala, ni changamoto kwa watoto wengi. Kuwapa taarifa mapema, kutumia ratiba zinazoonekana au kaunta za muda, na kuanzisha taratibu zinazojirudia husaidia mtoto kujiandaa kihisia. Kadri mtoto anavyojua kinachofuata, ndivyo anavyopunguza upinzani na hasira.

## Imarisha uhusiano na mtoto

Changamoto za kitabia huweza kudhoofisha uhusiano wa mzazi na mtoto endapo hazitashughulikiwa kwa hekima. Ndiyo maana ni muhimu mzazi kujenga muda wa ubora na mtoto, nje ya mazingira ya amri na adhabu.

Dakika chache kila siku za kucheza, kusikiliza au kuzungumza na mtoto bila kukosoa hujenga uaminifu na hupunguza migogoro. Mtoto anayehisi kusikilizwa na kuthaminiwa huwa tayari zaidi kushirikiana.

Pia, mzazi anapaswa kuangalia namna anavyodhibiti hisia zake mwenyewe, kwani watoto hujifunza kwa kuiga. Utulivu wa mzazi ni somo muhimu kwa mtoto katika kujifunza kudhibiti hisia zake.

## Tafuta msaada

Si changamoto zote za kitabia zinaweza kutatuliwa nyumbani. Endapo tabia ya mtoto inaathiri masomo, mahusiano na wenzake, au usalama wake na wa wengine, ni muhimu kutafuta msaada wa kitaalamu.

Baadhi ya watoto hukumbwa na changamoto ya kukosa umakini, na msukumo na kutotulia kupita kiasi, wasiwasi, matatizo ya kujifunza, tawahudi au athari za kiwewe, ambazo zinahitaji tathmini na msaada maalumu.

Kutafuta msaada si dalili ya kushindwa kwa mzazi, bali ni ishara ya kuwajibika. Kwa msaada sahihi, watoto huweza kujifunza stadi za kujidhibiti, kuwasiliana vyema na kukua katika mazingira yenye afya ya kihisia. Changamoto za kitabia, zikishughulikiwa kwa uelewa na subira, zinaweza kuwa fursa ya kumjenga mtoto na kuimarisha familia kwa ujumla.

UKHTI FATIMA SS




# Migogoro kama njia ya kuelekea mabadiliko

**Migogoro ni sehemu isiyoweza kuepukika katika maisha ya binadamu. Popote pale watu wanapokutana, kubadilishana mawazo, kufanya maamuzi au kushirikiana, tofauti za mitazamo na maslahi huibuka.**
**Kwa muda mrefu, migogoro imekuwa ikionekana kama jambo baya linalopaswa kuepukwa kwa gharama yoyote. Hata hivyo, mtazamo huu si sahihi kila wakati. Kwa hakika, migogoro inaweza kuwa kichocheo muhimu cha mabadiliko chanya, endapo itashughulikiwa kwa hekima na uelewa.**

## Vyanzo vya migogoro

Migogoro mara nyingi hutokana na sababu mbalimbali. Watu wana haiba tofauti, namna tofauti za kuwasiliana, na mitazamo tofauti kuhusu vipaumbele au malengo. Wengine hupata rasilimali au msaada kwa kiwango tofauti, hali inayoweza kuzua hisia za kutotendewa haki.

Aidha, viwango vya uwazi, uaminifu, na mitindo ya uongozi vinaweza kuchochea migongano. Mara nyingine, migogoro hutokana na historia ya maisha ya mtu au hamu ya kupinga ukosefu wa usawa uliopo katika jamii au taasisi.

Migogoro hujitokeza kwa sura tofauti. Kuna migogoro ya kawaida ya kimawazo, kama kutofautiana katika mbinu za kazi au mgongano wa vipaumbele. Pia kuna migogoro mikali zaidi kama matusi ya maneno, dharau au kupuuzwa, na katika hali mbaya zaidi, migogoro inaweza kugeuka kuwa vurugu za kimwili. Aina zote hizi zina ujumbe mmoja wa msingi: kuna jambo muhimu ambalo halijatatuliwa.

## Kuipuuza ni hatari

Jambo la hatari zaidi si migogoro yenyewe, bali ni kuipuuza au kuikwepa. Migogoro haitoweki kwa kupuuzwa; mara nyingi hukua kwa ukimya na kujirudia kwa nguvu zaidi baadaye.

Badala ya kuiogopa, ni muhimu kuitambua migogoro kama ishara ya hitaji la mabadiliko. Migogoro si adui — ni kichocheo cha mazungumzo, tafakuri na mageuzi.

Kushughulikia migogoro mara nyingi kunahitaji mazungumzo magumu. Mazungumzo haya yanaweza kuwa yasiyoepukika ili kufikia suluhisho la kudumu. Katika mazungumzo hayo, kwa kawaida tunalenga mojawapo ya matokeo matatu: suluhisho, mpango, au uelewa.

## Matokeo matatu

Matokeo ya kwanza na yanayofurahiwa zaidi ni kupata suluhisho kamili lakini haya ni matarajio makubwa, ukilinganisha na uhalisia. Tukizungumzia suluhu ni makubaliano ya kina yanayotarajiwa kudumu kwa muda mrefu na kwa kutekelezwa hayo matatizo mapya yataepukwa.

Ingawa suluhu inawezekana, si rahisi kuifikia mara moja. Hivyo, mnaweza kuishia kupata walau mpango fulani.

Mpango hauhitaji kutatua kila kitu mara moja, bali huweka mwelekeo wa pamoja. Hufafanua mipaka mipya, matarajio mapya, na namna ya kushughulikia changamoto zinazoendelea. Mpango huwekwa kwa vitendo zaidi ambavyo utekelezwaji wake hujenga daraja kati ya mgogoro wa sasa na suluhisho la baadaye.

Hata hivyo, hata huo mpango wakati mwingine hukosekana, hasa mwanzoni mwa mazungumzo, na hivyo mnaweza kufikia kupata uelewa wa pamoja kwa pande zote za mgogoro.

Uelewa ni uwezo wa kila mmoja kuona mgogoro kupitia macho ya mwenzako. Ni kutambua mahitaji, hofu, na matumaini ya pande zote. Uelewa hauondoi tofauti mara moja, lakini huondoa mzigo wa kihisia, huleta utulivu, na huweka msingi wa mpango au suluhisho la baadaye.

## Mgogoro, chachu ya mabadiliko?

Ili migogoro iwe chachu ya mabadiliko, tunahitaji kubadilisha mtazamo wetu. Badala ya kuiona kama vita ya kushinda au kushindwa, tunaweza kuiona kama fursa ya kuchunguza mitazamo inayokinzana. Migogoro inaweza kutulazimisha kujiuliza maswali magumu kuhusu tabia, maamuzi, au mifumo iliyopo. Kwa njia hii, migogoro hutusaidia kukua kama watu binafsi na kama jamii.

Hatua muhimu katika kushughulikia migogoro ni kuanza na kuunganisha uhusiano. Kutokubaliana na mtu hakumaanishi kumkosa heshima. Tukiruhusu tofauti za maoni zitufungie milango ya mawasiliano, basi pande zote hupoteza. Kuheshimiana, hata katikati ya tofauti, hufungua nafasi ya kujifunza na kuelewana.

Mwisho, ni muhimu kukumbuka kuwa hisia za migogoro zinaonyesha kuwa kuna jambo tunalojali. Kama tusingejali, kusingekuwa na mgogoro.

Kusikilizwa ni mojawapo ya mahitaji ya msingi ya binadamu. Watu wanapohisi wamesikilizwa, huwa tayari zaidi kuelewa, kubadilika, au hata kufanya maridhiano. Ingawa hatuwezi kumlazimisha mwenzetu awe tayari kwa mazungumzo magumu, tunaweza kudhibiti mtazamo na nia zetu wenyewe.

Wakati mwingine, hatua ya busara zaidi ni kuchukua muda, kujitenga kwa muda mfupi, na kurejea kwenye mazungumzo baadaye kwa moyo ulio tulivu. Migogoro ikishughulikiwa kwa hekima, inaweza kuwa daraja la kuelekea mabadiliko chanya na mahusiano bora zaidi.

NA UKHTI FATIMA



# Namna gani tunawahamasisha wafanyakazi wako

Katika taasisi yoyote, wafanyakazi ndio injini ya mafanikio. Pamoja na umuhimu wa mshahara na marupurupu, tafiti zinaonyesha wazi kuwa motisha ya kweli hutokana na namna mfanyakazi anavyohisi kuthaminiwa, kuendelezwa na kuheshimiwa. Makala hii inakuletea njia 31 zilizothibitishwa kisayansi za kujenga hamasa eneo la lolote la kazi.

## Utambuzi na kuthamini mchango wa mfanyakazi

Utambuzi ni chanzo kikubwa cha motisha kazini. Mfanyakazi anapothaminiwa kwa juhudi zake, hata pale anapofanya kazi ndogo au ya kawaida, hujenga hisia ya kuwa ana maana ndani ya taasisi.

Kutambua mafanikio madogo, kutoa pongezi za hadharani, na kuwa na tuzo kama "mfanyakazi wa mwezi" husaidia sana kuongeza ari ya kazi na kujenga ushindani chanya.

Vilevile, utambuzi haupaswi kutoka kwa viongozi pekee bali hata wenyewe kwa wenyewe. Mifumo ya wafanyakazi kutambuana wao kwa wao huimarisha mshikamano na kuheshimiana.

Kuadhimisha hatua binafsi kama siku za kuzaliwa, kumbukumbu za ajira au vyeti vya taaluma, pamoja na kutoa zawadi zenye maana kwa mfanyakazi, huonyesha kuwa taasisi inajali utu wa mfanyakazi, si kazi yake pekee.

## Ukuaji na maendeleo ya kitaaluma

Mfanyakazi anayejua ana nafasi ya kukua kitaaluma huwa na motisha ya ziada. Mikutano ya mara kwa mara ya ana kwa ana kati ya mfanyakazi na msimamizi wake hujenga uhusiano wa kuaminiana na kutoa fursa ya ushauri, tathmini na mwelekeo wa kazi. Kuweka malengo binafsi yanayolingana na dira ya taasisi hufanya mfanyakazi aone mchango wake una maana.

Zaidi ya hapo, mipango binafsi ya maendeleo, mafunzo ya ndani na nje, pamoja na masomo yanayolipiwa na kampuni, huongeza ujuzi na kujiamini.

Mafunzo ya kuvuka idara na kupandishwa vyeo ndani ya taasisi huonyesha wazi kuwa juhudi hulipwa, na kwamba mustakabali wa mfanyakazi unaweza kujengwa ndani ya taasisi hiyo hiyo.

## Uwiano wa kazi na maisha binafsi

Katika dunia ya kazi ya sasa, wafanyakazi wanathamini sana uwiano kati ya kazi na maisha binafsi. Ratiba za kazi zinazonenepa, kama muda unaonyumbulika au kazi ya mbali, huwasaidia wafanyakazi kutimiza majukumu yao ya kifamilia na kijamii bila kupunguza ufanisi kazini. Hali hii huongeza ari na kupunguza uchovu wa kudumu.

Kutoa mapumziko ya hiari na kuwekeza katika mipango ya ustawi wa mwili na akili ni njia nyingine muhimu ya motisha.

Mfanyakazi mwenye afya njema ya kimwili na kisaikolojia huwa na nguvu, umakini na moyo wa kujituma. Taasisi inayojali ustawi wa wafanyakazi wake hujenga uaminifu wa kudumu.

## Utamaduni chanya wa kazi

Utamaduni wa kazi una mchango mkubwa katika motisha ya wafanyakazi. Mawasiliano yaliyo wazi, ya mara kwa mara na yanayoheshimu pande zote hujenga mazingira ya kuaminiana. Viongozi wanaoonekana, wanaosikiliza na kuwa wazi katika maamuzi yao huwafanya wafanyakazi wajisikie kuwa sehemu ya taasisi, si watazamaji wa mbali.

Aidha, kusherehekea mila na mafanikio ya pamoja kazini, kuunda vikundi vya maslahi ya wafanyakazi, na kuhakikisha vifaa na zana za kazi ni za kisasa huongeza hamasa. Nidhamu inayotekelezwa kwa faragha, kusimamia wafanyakazi wanapokabili changamoto, na kuepuka upendeleo au undugu kazini huimarisha haki na heshima.

## Dumisha mazingira ya motisha kwa muda mrefu

Motisha haiishi kwa kuanzisha sera chache tu; ni mchakato endelevu. Taasisi zinapaswa kubaini mambo yanayokatisha tamaa wafanyakazi kwa kusikiliza mrejesho wao, na kuepuka mabadiliko yasiyo ya lazima yanayovuruga mifumo inayofanya kazi. Vilevile, kutoa taarifa mapema kuhusu mabadiliko huondoa hofu na upinzani.

Hatimaye, utamaduni mzuri wa kazi lazima ulindwe. Viongozi wanapaswa kuishi yale wanayohubiri, kufuatilia hali ya motisha ya wafanyakazi, na kufanya marekebisho pale inapobidi. Taasisi inayothamini watu wake hujenga wafanyakazi wenye ari, uaminifu na tija ya muda mrefu.